
THE REPUBLIC OF UGANDA
Ministry of Education and Sports

# ADVANCED SECONDARY CURRICULUM




# SILABASI YA FASIHI YA KISWAHILI

NCDC
NATIONAL CURRICULUM DEVELOPMENT CENTRE

2025

ADVANCED SECONDARY
CURRICULUM

# SILABASI YA FASIHI YA KISWAHILI

2025

Copyright © National Curriculum Development Centre, Uganda 2025

A product of the National Curriculum Development Centre for the Ministry of Education and Sports with support from the Government of Uganda

National Curriculum Development Centre
P.O. Box 7002,
Kampala- Uganda
www.ncdc.co.ug

**ISBN: 978-9970-494-95-8**

All rights reserved: No part of this publication may be reproduced, stored in a retrieval system or transmitted in any form or by any means, electronic, mechanical, photocopying, recording, or otherwise, without the prior permission of the copyright holder

# YALIYOMO

**Dibaji** ........ v
**Shukrani** ........ vi
**1.0 Utangulizi** ........ 1
1.1 Mabadiliko katika Mtaala ........ 1
1.2 Tathmini ya Darasani ........ 2
1.3 Wanafunzi wenye Mahitaji Maalumu ya Kielimu ........ 2
1.4 Stadi za Msingi ........ 3
1.5 Masuala Mtambuka ........ 4
1.6 Maadili ........ 4
1.7 Matumizi ya TEHAMA ........ 4
1.8 Miradi ........ 5
1.9 Madhumuni ya Elimu ya Sekondari ........ 5
1.10 Malengo ya Mtaala wa Sekondari ya Juu ........ 6
1.11 Sababu za Kufundisha Fasihi ya Kiswahili katika Shule za Sekondari ya Juu ........ 6
1.12 Maelezo kuhusu Mafunzo ........ 7
1.13 Muda ........ 7
1.14 Mbinu Pendekezwa za Kufundishia Fasihi ya Kiswahili ........ 7
1.15 Upeo na Mfuatano wa Mada ........ 7
**2.0 SILABASI KAMILI YA FASIHI YA KISWAHILI** ........ 10
**Kidato Cha Tano Muhula Wa Kwanza** ........ 10
Mada 1.1: Nathari ........ 10
Mada 1.2: Ushairi ........ 12
Mada 1.3: Tamthilia ........ 14
Mada 1.4: Riwaya ........ 15
**Kidato Cha Tano Muhula Wa Pili** ........ 17
Mada 2.1: Nathari ........ 17
Mada 2.2: Ushairi ........ 18
Mada 2.3: Tamthilia ........ 20
Mada 2.4: Riwaya ........ 21
**Kidato Cha Tano Muhula Wa Tatu** ........ 22
Mada 3.1: Nathari ........ 22
Mada 3.2: Ushairi ........ 24
Mada 3.3: Tamthilia ........ 25

Mada 3.4: Riwaya ... 27

**Kidato Cha Sita Muhula Wa Kwanza ... 28**

Mada 1.1: Nathari ... 28

Mada 1.2: Ushairi ... 29

Mada 1.3: Tamthilia ... 30

Mada 1.4: Riwaya ... 31

**Kidato Cha Sita Muhula Wa Pili ... 32**

Mada 2.1: Nathari ... 32

Mada 2.2: Ushairi ... 33

Mada 2.3: Tamthilia ... 34

Mada 2.4: Riwaya ... 35

**Kidato Cha Sita Muhula Wa Tatu ... 36**

Mada 3.1: Nathari ... 36

Mada 3.2: Ushairi ... 37

Mada 3.3: Tamthilia ... 38

Mada 3.4: Riwaya ... 39

**3.0 Tathmini ya Fasihi ya Kiswahili ... 40**

3.1 Kutathmini Matarajio mapya ya Ujifunzaji ... 40

3.2 Mitihani ... 40

3.3 Tathmini Endelevu ... 40

3.4 Stadi za Msingi ... 41

3.5 Maadili/ Mitazamo ... 41

**Sherehe ... 42**

# DIBAJI

Wizara ya Elimu na Michezo, kupitia Taasisi ya Kitaifa ya Ukuzaji Mitaala *(National Curriculum Development Center - NCDC)* imerekebisha mtaala wa sekondari ya juu (Kidato cha tano na cha sita) kwa azma ya kuufungamanisha na ule wa shule za sekondari ya chini (Kidato cha kwanza hadi cha nne). Mtaala huu wa Fasihi ya Kiswahili ni sehemu ya mtaala ambao umerekebishwa na kupangwa kuwatayarisha wanafunzi kukuza na kuendeleza stadi zao, kujiendeleza kikazi, kimaisha na kuwawezesha kuchangia maendeleo ya nchi yetu na dunia kwa jumla.

Mtaala huu ambao umerekebishwa unalenga kuwezesha wanafunzi ambao wamehitimu ngazi ya sekondari ya chini, kuendeleza waliyoyasoma katika ngazi ya chini kwa kuzingatia mikabala ya ufundishaji, ujifunzaji na utathmini. Kwa hiyo, mtaala huu unalenga kuendeleza umilisi wa Kiswahili kwa kila mwanafunzi. Mtaala huu unawapa wanafunzi fursa ya kuimarisha ukuzaji na uendelezaji wa stadi za karne ya 21 pamoja na stadi za msingi ambazo wanafunzi walijifunza katika ngazi ya sekondari ya chini. Mtaala huu unawatayarisha wanafunzi kudhihirisha maendeleo ya matumizi ya yale waliyojifunza ili kutatua changamoto zinazohusiana na uchumi wa kijamii. Hii ndiyo sababu mtaala huu unasisitiza suala la wanafunzi kuhusika katika shughuli za kijamii kama sehemu mojawapo ya ujifunzaji.

Mtaala huu wa Fasihi ya Kiswahili unaendeleza matumizi ya ujuzi, ufahamu na stadi ambazo wanafunzi walijifunza awali, ili kuzitumia katika kutatua changamoto wanazokumbana nazo katika maisha ya kawaida. Maendeleo yao katika viwango hivi vya ujifunzaji huwawezesha kukuza stadi za msingi, kama vile; mawasiliano bora, utafakari na utatuzi wa matatizo. Aidha, unakuza uwezo wao wa kupata stadi za tafakuri kama vile, udadisi, ubunifu na uvumbuzi, uamuzi na utafakari. Mtaala huu unapendekeza matumizi ya mbinu za ufundishaji zinazowashirikisha wanafunzi katika shughuli zifungamanazo na tajriba za hali halisi za maisha pamoja na kuthamini viwango mbalimbali vya wanafunzi wenye uwezo tofauti wa ujifunzaji.

Kwa hiyo, naidhinisha mtaala huu kama hati rasmi ya kutumia katika ufundishaji na ujifunzaji wa Fasihi ya Kiswahili kwenye ngazi ya sekondari ya juu nchini Uganda.



Mhe. Janet Kataaha Museveni

**Waziri wa Elimu na Michezo**

## SHUKRANI

Taasisi ya Kitaifa ya Ukuzaji Mitaala inaishukuru Serikali ya Uganda kwa kufadhili mchakato wa urekebishaji wa mtaala wa sekondari ya juu nchini Uganda.

Tunaishukuru Wizara ya Elimu na Michezo kwa kusimamia urekebishaji wa mtaala. Kikosikazi kutoka Wizara ya Elimu na Michezo, kwa kusimamia urekebishaji wa mtaala huu na kufanya maamuzi yalipohitajika na kwa muda mwafaka, tunawashukuru sana.

Shukrani za dhati ziwaendee wanajamii ambao walichangia maoni muhimu sana katika kurekebisha mtaala huu. Jitihada zao katika kuhakikisha kuwa mtaala huu unatumiwa katika shule za upili nchini Uganda zilifaa sana.

NCDC pia inawashukuru washikadau wote mkiwemo wabunge, shule, vyuo na taasisi nyingine za elimu ya juu, ambao walichangia kwenye urekebishaji na muundo wa mtaala huu wa elimu ya sekondari ya juu. Aidha, NCDC inawashukuru wanajopo na wanataaluma mbalimbali kwa mchango wao kwa kazi hii.

Mwisho, NCDC inawashukuru wale wote ambao majina yao hayajatajwa wala kuoneshwa katika hati hii lakini walichangia kukamilika kwa mtaala huu.

NCDC inachukua lawama zote kwa mapungufu yaliyomo katika mtaala huu na inakaribisha mapendekezo chanya ya kuuboresha zaidi. Maoni na mapendekezo yanaweza kuwasilishwa kwa NCDC kupitia S.L.P 7002, Kampala au Anwanipepe: admin@ncdc.go.ug au kwenye tovuti: www.ncdc.go.ug

Dkt. Grace K. Baguma

Mkurugenzi

**Taasisi ya Kitaifa ya Ukuzaji Mitaala**

# 1.0 UTANGULIZI

Kwa mujibu wa katiba ya nchi ya Jamhuri ya Uganda ibara 6(2), Lugha ya Kiswahili ndiyo lugha rasmi ya pili nchini na pia imetamkwa kama *lingua franca* katika kifungu 137 cha Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (JAM). Aidha, mkutano wa tarehe 22 Julai, 2022 wa viongozi wa nchi za JAM uliidhinisha Kiswahili kuwa mojawapo ya lugha rasmi za Jumuiya. Uganda kama nchi mwanachama ina wajibu wa kuendeleza Lugha ya Kiswahili kwa ajili ya maendeleo endelevu ya kikanda. Kwa hivyo, serikali ya Uganda kupitia Wizara ya Elimu na Michezo imefadhili uandaji wa mitaala ya Kiswahili kwa ngazi mbalimbali za kielimu. Pamoja na hilo, imewezesha urekebishaji wa mtaala wa Sekondari ya juu ambao umepangwa upya ili kuufungamanisha na ule wa ngazi ya sekondari ya chini ambao umeegemezwa kwa mkabala wa umilisi ili kurahisisha maendeleo ya wanafunzi kutoka kiwango cha chini hadi cha juu. Ufungamanishaji wa mtaala huu umetokana na uchambuzi ambao umefanywa kutokana na mtaala wa ngazi ya sekondari ya juu ambao umekuwepo tangu ulipochapishwa 2013. Uchambuzi huu ulilenga kutambua ikiwa mtaala huu:

i) unafaa.
ii) ni wa kiwango cha juu au una mada nyingi kuzidi kiasi.
iii) una mada ambazo zilifundishwa katika ngazi ya sekondari ya chini.
iv) una mada ambazo hazifai tena au zimepitwa na wakati.
v) una mada ambazo zinarudiwarudiwa.

Matokeo ya uchambuzi huu wa mtaala yalionesha kwamba kulikuwa na dhana nyingi ambazo zinajirudiarudia katika mada kadhaa ambazo zimefunzwa katika ngazi ya sekondari ya chini. Pamoja na hayo, kulikuwa na dhana ambazo hazihitajiki tena katika jamii ya karne ya 21. Haya yote yalisababisha wingi wa mada ambazo zilijaza mtaala.

## 1.1 Mabadiliko katika Mtaala

Ufungamanishaji wa mtaala wa ngazi ya sekondari ya juu na ule wa ngazi ya sekondari ya chini ulisababisha mabadiliko katika mbinu za ufundishaji ambazo awali zilikuwa zimeegemea mkabala wa maarifa na malengo na kuufanya uwe wa kujumuisha na kushirikisha wanafunzi katika somo, ambao unajulikana kama mkabala wa kiumilisi. Kwa hiyo, silabasi hii iliyorekebishwa imetokana na umantiki, ujumlishaji na uunganishaji wa mada ambazo zilikuwa zinajirudiarudia. Aidha, iliangazia stadi zinazofanana, udondoshaji wa mada ambazo zilikuwa zimesomwa katika ngazi ya sekondari ya chini, au zile mada ambazo zilikuwa hazifai tena kukidhi mahitaji ya ujifunzaji wa karne ya 21. Vilevile, ulilenga kuboresha yale ambayo yalikuwa na umilisi wa chini na kuyafanya yalingane na kiwango cha juu. Mchakato wa ufunzaji na ujifunzaji umeoneshwa vizuri katika upeo na mfuatano wa mada, ukizingatia utaratibu wa maendeleo ya mafunzo ambayo yanatokana na matarajio ya ujifunzaji na mbinu za utathmini. Ukurasa wenye silabasi kamilifu unaangazia tajriba zote za ujifunzaji na matokeo yanayotarajiwa kama mchakato wa ujifunzaji.

Silabasi hii ya Kiswahili ni sehemu ya mtaala uliorekebishwa na kuchapishwa kwa ajili ya wanafunzi wanaojiunga na sekondari ya juu ambao wamekuwa wakisoma kufuatana na mtaala wa sekondari ya chini uliorekebishwa. Ni muhimu kusoma silabasi nzima kabla hujapanga mipango yako ya kufundisha kwa kuwa baadhi ya mada zimeboreshwa. Wakati wa kufungamanisha silabasi hii, jitihada zilifanywa za kuhakikisha mwendelezo kutoka ngazi ya chini, kurekebisha mada na mafunzo yenye sifa zinazofanana ambazo ni za thamani kwa maisha ya mwanafunzi na jamii kwa ujumla. Zaidi ya hayo, mchakato wa kuendeleza mtaala huu ulidondosha mada na dhana ambazo zilichukuliwa kuwa zimepitwa na wakati, ziko kwa kiwango cha juu au zinajirudiarudia au ni nyingi zaidi.

## 1.2 Tathmini ya Darasani

Silabasi hii inahitaji ujifunzaji wa darasani kuhusishwa na tajriba za wanafunzi kupitia shughuli pendekezwa za ujifunzaji ili kupata matokeo tarajiwa ya mafunzo. Hiki ndicho kiini cha mtaala wenye mkabala unaozingatia mbinu na shughuli zinazoshirikisha mwanafunzi katika ujifunzaji ili kupata umilisi unaohitajika. Tathmini endelevu ya Fasihi ya Kiswahili inalenga upataji wa ujuzi na stadi kupitia utendaji wa shughuli za ujifunzaji. Shughuli za ujifunzaji zinaibuka kutoka matarajio ya ujifunzaji ambayo yanathibitishwa na upataji na udhihirishaji wa matumizi ya stadi zinazotarajiwa ili kuthibitisha kwamba ujifunzaji umetendeka. Mifano ya tathmini pendekezwa imetolewa kumwongoza mwalimu kufanya tathmini ya darasani. Mwalimu anaweza kutumia mbinu nyingine za utathmini kwa kuegemea kanuni zile tatu za uchunguzaji, uzungumzaji na matokeo ya ujifunzaji kwa lengo la kupata ujuzi tarajiwa, stadi, maadili na mitazamo.

(**Rejelea silabasi kamili)**

## 1.3 Wanafunzi wenye Mahitaji Maalumu ya Kielimu

Mtaala uliorekebishwa umeundwa kuwezesha wanafunzi wote, mkiwemo wale wenye mahitaji maalumu ya kielimu, kutumia uwezo wao na kuchangia maendeleo ya nchi. Kwa kuingiza na kuzingatia mikakati na mbinu zinazohusisha wote, mtaala huu unahakikisha usawa wa kila mwanafunzi kupewa fursa za kupata elimu nzuri na kuhifadhi kiwango cha juu cha elimu. Mtaala unasisitiza mazingira wezeshi ya ujifunzaji kwa wanafunzi wote mkiwemo na wale walio na mahitaji tofauti tofauti ya kielimu kwa kuwawezesha kufaulu kama wenzao.

## 1.4 Stadi za msingi

Stadi za msingi si masomo tofauti, bali ni kiini cha kila somo. Ni stadi zinazomwezesha mwanafunzi kupata na kuimarisha maarifa katika mtaala mzima. Stadi hizi zimejumuishwa ndani ya matokeo ya ujifunzaji na katika shughuli za mafunzo za masomo mbalimbali. Stadi za msingi na viashiria vyake zimeonyeshwa hapa chini:

Stadi hizi humwezesha mtu kubadilika kufuatana na mabadiliko ili kuweza kukabiliana na changamoto za kimaisha za karne ya 21.

1

**Kutafakari na Utatuzi wa Matatizo**
i) Kupanga na kutekeleza uchunguzi.
ii) Kupanga na kuchambua taarifa.
iii) Kutambua matatizo na njia za kuyatatua.
iv) Kutabiri matokeo na kufanya maamuzi yenye mantiki.
v) Kutathmini masuluhisho mbalimbali.

2

**Ushirikiano na Ujifunzaji wa Kujitegemea**
i) Kufanya kazi kwa ufanisi katika timu mbalimbali.
ii) Kushirikiana kwa ufanisi na wengine.
iii) Kuwajibika kwa ujifunzaji binafsi.
iv) Kufanya kazi kwa kujitegemea na kwa ustahimilivu.
v) Kudhibiti malengo na muda.

3

**Ubunifu na Uvumbuzi**
i) Kutumia ubunifu kuchunguza masuala mbalimbali ya uwezekano.
ii) Kushirikiana na wengine ili kuzalisha mawazo.
iii) Kupendekeza na kuendeleza masuluhisho mapya.
iv) Kujaribu mbinu mbadala za kibunifu.
v) Kuchunguza mifumo na kufanya mahitimisho ya jumla.

4

**Mawasiliano**
i) Kusikiliza kwa makini na kwa ufahamu.
ii) Kuzungumza kwa kujiamini na kueleza mawazo/maoni kwa uwazi.
iii) Kusoma kwa usahihi na kwa ufasaha.
iv) Kuandika na kuwasilisha kwa mpangilio mzuri.
v) Kutumia njia mbalimbali za mawasiliano kueleza mawazo.

5

**Mahesabu na Makokotoo ya Hisabati**
i) Kutumia namba na vipimo kwa usahihi.
ii) Kutafsiri na kuchunguza takwimu za hisabati.
iii) Kutumia hisabati kufafanua na kuendeleza maamuzi.

6

**Umilisi katika matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA)**
i) Kutumia teknolojia kuunda, kurekebisha, na kuchakata taarifa.
ii) Kutumia teknolojia kushirikiana, kuwasiliana, na kuboresha kazi.

7

**Utofauti na kuthamini Tamaduni Mbalimbali**
i) Kuthamini utofauti wa tamaduni.
ii) Kujibu kwa heshima kwa watu wa tamaduni zote.
iii) Kuheshimu mila na desturi chanya za kitamaduni.
iv) Kutambua uasilia wa kikabila kama chimbuko la ubunifu na uvumbuzi.

## 1.5 Masuala Mtambuka

Haya ni masuala ambayo wanafunzi huhitaji kuyajua na kujifunza. Hayafungwi kwa somo moja mahsusi bali yanazingatiwa katika masomo yote. Yanasaidia wanafunzi kufahamu mshikamano uliopo kati ya masomo mbalimbali na changamoto zinazopatikana maishani. Haya ni:

i) utambuzi wa mazingira.
ii) utambuzi wa masuala ya kiafya.
iii) stadi za kimaisha.
iv) uwezo tofauti tofauti na uhusikaji.
v) changamoto za kijamii na kiuchumi.
vi) uraia na uzalendo.

Haya yanahusu kila binadamu bila kujali masomo yao mahsusi ya kitaaluma. Yanapatikana ndani ya matarajio ya mafunzo mbalimbali.

## 1.6 Maadili

Mtaala huu umejengeka kwenye maadili thabiti. Maadili haya ndiyo msingi wa mtaala huu na ni dhima ya shule kuyaendeleza. Wanafunzi wanapaswa kujiegemeza kwa maadili haya kama wananchi wa Uganda. Maadili haya yanatokana na Sera ya Maadili ya Kitaifa ya Uganda ya 2013. Haya ni pamoja na:

i) heshima kwa binadamu na mazingira.
ii) kuwa mwaminifu kila wakati.
iii) haki na usawa kwa wengine.
iv) jitihada za kazi ili kijitegemea.
v) uadilifu, kujiendeleza vizuri na wema.
vi) ubunifu na uvumbuzi.
vii) kuwajibika kijamii.
viii) mtagusano wa kijamii.
ix) umoja wa kitaifa.
x) thamani ya kitaifa na uzalendo.

Maadili haya hayafundishwi moja kwa moja katika masomo wala hayatathminiwi kwa kutumia kalamu na karatasi bali yamo ndani ya matarajio ya ujifunzaji na hukuzwa pindi mwanafunzi anavyoendelea kujifunza.

## 1.7 Matumizi ya TEHAMA

Matumizi ya vyombo vya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika ufundishaji na ujifunzaji wakati wa kutekeleza mtaala huu, yanahimizwa sana. Matumizi ya teknolojia katika ufunzaji na ujifunzaji ni suala nyeti katika kutekeleza mtaala wa umilisi kwa sababu yanavutia na kuhimiza ushiriki wa wanafunzi, ubunifu wao na ujifunzaji wa kudumu maishani. Walimu wanahimizwa kutumia vyombo vya TEHAMA ili kuzalisha mafunzo shirikishi kama vile maigizo ya kidijitali na video ambayo yatarahisisha uelewa wa mada na dhana dhahania na kuzifanya

kuonekana hai na halisi. Mchanganyiko wa mbinu za ufundishaji unaweza kutumiwa pamoja na majukwaa ya kujifunzia mtandaoni kama vile, *Google Classroom, Zoom, Microsoft Teams, YouTube, Google Docs,* n.k., kuimarisha ushirikiano na kuwasilisha majibu yaliyobinafsishwa. Matumizi ya TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji hayataimarisha tajriba ya ujifunzaji pekee bali yatawezesha wanafunzi kukuza stadi za kutafakari kidijitali kama inavyohitajika katika karne ya 21.

## 1.8 Miradi

Miradi na matumizi ya miradi kama mbinu ya ufundishaji ni sehemu nyeti katika ujifunzaji wa karne ya 21. Katika Fasihi ya Kiswahili, mwanafunzi anahitajika kuandaa matini za kusoma, hadithi, mashairi, nyimbo, miswada ya kuigiza, sura za riwaya, n.k., kama miradi ya somo hili. Miradi hii itamchochea mwanafunzi kufanya utafiti wa kiakademia na kuendeleza stadi za kuandika na kubuni kuhusu mada yoyote ya hiari yake. Walimu wanahimizwa kuongoza wanafunzi kushiriki katika miradi ambayo inaweza kuunganishwa kwa urahisi na yale masuala halisi yanayotendeka katika jamii zao. Uandishi wa matini za kusoma utampa mwanafunzi fursa ya kushiriki katika utafiti akiongozwa na mwalimu na baadaye atawasilisha andiko lake lenye umbo zuri na lenye kuwakilisha mawazo yake.

## 1.9 Madhumuni ya Elimu ya Sekondari

Madhumuni ya elimu ya sekondari nchini Uganda ni:

i) kuimarisha na kuendeleza umoja wa kitaifa, uelewa wa majukumu ya kijamii na uraia, upendo thabiti na huduma kwa wengine, na heshima kwa mali ya umma, pamoja na kuthamini uhusiano wa kimataifa;

ii) kuendeleza thamani na ufahamu wa urithi wa kitamaduni wa Uganda mkiwemo lugha zake;

iii) kufunza na kuendeleza hisia za kujiheshimu, maadili, uwajibikaji wa kibinafsi na kujituma;

iv) kuwawezesha watu kupata na kuendeleza ujuzi na ufahamu wa mahitaji ibuka ya jamii na uchumi;

v) uwezeshaji wa maarifa ya kisasa na ya kina kupitia vipengele vya kinadharia na vya kimatendo vya uzalishaji wenye ubunifu, mbinu za kisasa za usimamizi katika uwanja wa biashara na viwanda, na matumizi yake katika muktadha wa maendeleo ya kijamii na kiuchumi nchini uganda;

vi) kuwawezesha watu kupata maarifa ya msingi ya kisayansi, teknolojia, taaluma, kilimo na stadi za kibiashara zinazohitajika kwa mtu kujianzishia biashara.

vii) kuwawezesha watu kukuza stadi za kibinafsi kama vile utatuzi wa matatizo, ukusanyaji wa taarifa na kuzifasiri, kujitegemea binafsi wanaposoma na kuandika, kujiendeleza kupitia ujifunzaji na uendelezaji wa stadi za kijamii, kimwili na kiuongozi kama zile zinazokuzwa kupitia michezo, mashirika na vyama;

viii) kuweka msingi wa kujiendeleza kielimu;

ix) kumwezesha mtu kutumia stadi alizojifunza katika kutatua matatizo ya jamii na kujenga hisia imara za ujenzi wa jamii na kujitambulisha na jamii yake;

x) kuimarisha mitazamo kuhusu ufanyaji kazi na heshima thabiti ya ufanyaji kazi na wale wanaofanya kazi kuhakikisha maendeleo ya nchi yanatimia;

xi) kukuza na kuendeleza mitazamo chanya kuhusu ujifunzaji kama mchakato mrefu wa kimaisha.

## 1.10 Malengo ya Mtaala wa Sekondari ya Juu

Malengo ya sekondari ya juu ni;

i) Kuendeleza mtaala wenye mkabala wa umilisi.
ii) Kuendeleza elimu ya jumla kwa maendeleo ya kila mtu na kitaifa kwa kuegemea maadili ya wote.
iii) Kuendeleza stadi muhimu za ajira, za maisha na kuendeleza ujifunzaji endelevu.
iv) Kutumia mkabala jumlishi wa ujifunzaji ambao huendeleza uwezo wa wanafunzi wa kutumia waliyojifunza.
v) Kuboresha utathmini endelevu wa shuleni hadi utathmini tamati.
vi) Kusisitiza ushiriki wa wanafunzi katika shughuli za jamii.
vii) Kujitayarisha kuendelea na masomo ya juu.

## 1.11 Sababu za Kufundisha Fasihi ya Kiswahili katika Shule za Sekondari ya Juu

Silabasi ya sekondari ya juu inalenga kuwawezesha mwanafunzi wa fasihi ya Kiswahili:

i) kujieleza kwa ufasaha na kujiamini ili kuwasilisha mawazo yake kwa uwazi.
ii) kutumia mawasiliano bora kulingana na hadhira anayowasiliana nayo.
iii) kufafanua, kuchambua, kuhakiki, kutathmini na kueleza mawazo yake na ya wasomi mbalimbali kulingana na kazi za kifasihi ambazo amekumbana nazo.
iv) kukuza na kuendeleza stadi mbalimbali za kimaisha na za msingi ili aweze kutafakari, kutatua matatizo, kuwasiliana ipasavyo na kushirikiana vyema na wanajamii wenzake.
v) kubuni kazi mbalimbali za kisanaa ili kupanua ujuzi wake, utendaji na kujipatia kipato cha kujikimu maishani.

## 1.12 Maelezo kuhusu Mafunzo

Maeneo ya masomo yamepangwa upya katika silabasi kuibuka na mtaala uliorekebishwa. Silabasi ya Fasihi ya Kiswahili iliyorekebishwa imepangwa kwa mada nne, yaani, Nathari, Ushairi, Tamthilia na Riwaya. Hizi ndizo mada ambazo zinajitokeza kila muhula katika silabasi nzima.

Hata hivyo, ingawa mada zinabaki zizo hizo, viwango vya ujifunzaji vinaendelea kupanuka. Kwa mfano, kiwango cha ujifunzaji katika muhula wa kwanza kinakuwa rahisi ukilinganisha na muhula wa pili au wa tatu mfululizo. Kwa hiyo, mafunzo yamepangwa kwa utaratibu ili kuwezesha mwanafunzi kuendeleza masomo yake kiutaratibu.

## 1.13 Muda

Wanafunzi watashirikishwa kwa vipindi tisa kila wiki, yaani vipindi vitatu kwa mada ya Nathari na Ushairi, vipindi vitatu kwa mada ya Tamthilia na vipindi vitatu kwa mada ya Riwaya kutoka kidato cha tano hadi cha sita.

## 1.14 Mbinu Pendekezwa za Kufundishia Fasihi ya Kiswahili

Mbinu ambazo zinapendekezwa ni zile ambazo zinashirikisha wanafunzi katika somo. Mtaala huu umependekeza baadhi ya mbinu ambazo mwalimu anaweza kutumia kufundisha wanafunzi. Lakini, kama ilivyotajwa, mbinu zimependekezwa, kwa maana, si za lazima. Mwalimu ana uhuru wa kutumia mbinu zozote zile kulingana na mazingira, uwezo na kuhakikisha kwamba zinashirikisha wanafunzi. Mifano ya mbinu ambazo zimependekezwa zimo katika silabasi.

## 1.15 Upeo na Mfuatano wa Mada

| Kidato/ Muhula | Mada | Mada ndogo | Vipindi |
|---|---|---|---|
| Kidato cha Tano<br><br>Muhula wa Kwanza | Nathari | Utangulizi wa fasihi | 2 |
| | | Aina za fasihi | 2 |
| | | Dhima ya fasihi katika jamii | 2 |
| | | Aina za nathari | 2 |
| | | Uainishaji wa hadithi | 3 |
| | | | **11** |
| | Ushairi | Utangulizi wa ushairi wa Kiswahili | 3 |
| | | Istilahi za kishairi | 3 |
| | | Aina za mashairi | 4 |
| | | | **10** |
| | Tamthilia | Utangulizi wa tamthilia | 4 |
| | | Uainishaji wa tamthilia | 05 |
| | | Vipengele vya tamthilia<br>-maudhui | 12 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | -wahusika | |
| | | | **21** |
| | Riwaya | Utangulizi wa riwaya | 4 |
| | | Aina za riwaya | 5 |
| | | Vipengele vya riwaya<br>-maudhui<br>-wahusika | 12 |
| | | | **21** |
| **JUMLA** | | | **63** |
| Kidato cha Tano<br><br>Muhula wa Pili | Nathari | Matumizi ya lugha | 10 |
| | | Mtindo | 8 |
| | | | **18** |
| | Ushairi | Muundo wa shairi<br>-Umbo (mada, beti, mishororo) | 06 |
| | | Ujumbe wa shairi | 06 |
| | | Mbinu za kishairi | 06 |
| | | | **18** |
| | Tamthilia | Vipengele vya Tamthilia<br>-Matumizi ya lugha | 36 |
| | | | **36** |
| | Riwaya | Mbinu za Usimulizi | 18 |
| | | Matumizi ya lugha | 18 |
| | | | **36** |
| **JUMLA** | | | **108** |
| Kidato cha Tano<br><br>Muhula wa Tatu | Nathari | Mtazamo katika nathari | 09 |
| | | Dhamira | 09 |
| | | | **18** |
| | Ushairi | Bahari za ushairi | 18 |
| | | | **18** |
| | TAMTHILIA | Mbinu za uigizaji wa tamthilia | 24 |
| | | Maleba | 12 |
| | | | **36** |
| | Riwaya | Mgogoro | 12 |
| | | Wahusika | 12 |
| | | Maudhui | 12 |
| | | | **36** |
| **JUMLA** | | | **108** |
| Kidato cha Sita<br><br>Muhula wa Kwanza | Nathari | Mbinu za uandishi wa nathari | 04 |
| | | Utunzi wa kazi za nathari | 14 |
| | | | **18** |
| | Ushairi | Utunzi na uwasilishaji wa mashairi | **18** |
| | | | **18** |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | Tamthilia | Mgogoro | 26 |
| | | Maelezo ya jukwaa | 10 |
| | | | **36** |
| | Riwaya | Utunzi wa sura ya/za riwaya | 36 |
| | | | **36** |
| **JUMLA** | | | **108** |
| Kidato cha Sita<br><br>Muhula wa Pili | Nathari | Uchambuzi wa matumizi ya lugha | 18 |
| | | | 18 |
| | Ushairi | Uchambuzi wa hali, hisia, sauti ya mzungumzaji na toni katika mashairi | 18 |
| | | | **18** |
| | Tamthilia | Utunzi wa tamthilia | 18 |
| | | Uigizaji wa tamthilia | 18 |
| | | | **36** |
| | Riwaya | Mandhari | 16 |
| | | Ploti | 20 |
| | | | **36** |
| **JUMLA** | | | **108** |
| Kidato cha Sita<br><br>Muhula wa Tatu | Nathari | Uchambuzi wa kina wa kazi za nathari | 10 |
| | | | **10** |
| | Ushairi | Uchambuzi wa kina wa mashairi | **11** |
| | | | **21** |
| | Tamthilia | Uchambuzi wa kina wa tamthilia | 21 |
| | | | **21** |
| | Riwaya | Uchambuzi wa kina wa riwaya | 21 |
| **JUMLA** | | | **63** |

# 2.0 SILABASI KAMILI YA FASIHI YA KISWAHILI

## Kidato Cha Tano Muhula Wa Kwanza

### MADA 1.1: Nathari

**Vipindi** 11

**Umilisi jumuishi:** Mwanafunzi achanganue na kubuni kazi mbalimbali za nathari kwa kuzingatia vipengele vya kifasihi ili kuimarisha ustadi wa kuandika na mawasiliano bora.

| **Matarajio ya Ujifunzaji**<br>Mwanafunzi aweze: | **Shughuli Pendekezwa za Mafunzo** | **Sampuli ya Tathmini** |
|---|---|---|
| a) kudhihirisha uelewa wa dhana ya fasihi na dhima yake katika jamii. (u, s, a) | a) Ongoza wanafunzi katika vikundi kubunguabongo kuhusu dhana ya fasihi na aina zake na kuwasilisha maoni yao darasani.<br><br>b) Katika vikundi au jozi, wape wanafunzi matini mbalimbali za tanzu tofauti za fasihi k.v; shairi, riwaya, tamthilia na kuwaagiza kufanya utafiti kuhusu sifa za matini hizo na kuwasilisha matokeo yao darasani.<br><br>c) Elekeza wanafunzi katika vikundi kuteua utanzu mmoja wa fasihi na kufanya utafiti kuhusu dhima yake katika jamii na kuwasilisha matokeo yao darasani. | a) Angalia na kutathmini wanafunzi katika vikundi au jozi wakishirikiana;<br>• Kubunguabongo kuhusu dhana ya fasihi na aina zake.<br>• Kufafanua sifa za tanzu mbalimbali za fasihi.<br>• Kujadili dhima ya fasihi katika jamii.<br>b) Zungumza na wanafunzi na kuwauliza maswali ili kutambua uelewa wao kuhusu;<br>• Dhana ya fasihi.<br>• Tanzu za fasihi.<br>• Dhima ya fasihi katika jamii.<br>c) Mawasilisho ya wanafunzi darasani kuhusu dhana ya fasihi, tanzu za fasihi na dhima yake katika jamii. |

| | | |
|---|---|---|
| b) kubainisha aina mbalimbali za nathari kwa kutofautisha sifa zake kuu na tanzu nyinginezo za kifasihi. *(u, s, gs)* | a) Katika vikundi, elekeza wanafunzi kubunguabongo kuhusu dhana ya nathari kisha wafanye mawasilisho darasani.<br><br>b) Wape wanafunzi matini mbalimbali za nathari wazisome na kutambua aina zake na kufanya mawasilisho.<br><br>c) Weka wanafunzi katika vikundi viwili, kikundi kimoja kipewe matini ya nathari na kingine kipewe matini ya kishairi. Kila kikundi kitambue sifa za matini husika na kufanya mawasilisho darasani. | a) Angalia wanafunzi wakibunguabongo kuhusu dhana ya nathari kutathmini ustadi wao wa kujieleza kwa ujasiri.<br>b) Zungumza na wanafunzi ukiwadadisi kuhusu;<br>• aina mbalimbali za nathari.<br>• tofauti kati ya nathari na ushairi.<br>c) Tathmini mawasilisho ya wanafunzi na kazi zao andishi kuthibitisha uelewa wao wa:<br>• maana ya nathari na uainishaji wake.<br>• sifa za nathari na tofauti yake na ushairi. |
| c) kuainisha hadithi mbalimbali na kuchanganua sifa zake. *(u, s, gs)* | a) Katika vikundi au jozi, shirikisha wanafunzi;<br>kubunguabongo kuhusu aina mbalimbali za hadithi na kuwasilisha maoni yao darasani.<br><br>b) Elekeza wanafunzi katika vikundi au jozi kusoma hadithi mbalimbali na kufafanua aina zake.<br>c) Ongoza wanafunzi katika vikundi au jozi kusoma hadithi teule na kujadili sifa zake<br>d) Ongoza wanafunzi kutunga au kusimulia hadithi yoyote kwa kuzingatia sifa bainifu za hadithi hiyo. | a) Angalia wanafunzi na kutathmini uwezo wao wa kushirikiana katika vikundi kueleza aina za hadithi.<br><br>b) Uliza wanafunzi maswali ya kuchochea ili kuthibitisha majibu yao kuhusu sifa za hadithi teule.<br><br>c) Tathmini masimulizi au hadithi za wanafunzi walizotunga kwa kuzingatia;<br>• aina ya hadithi<br>• sifa za hadithi |

## MADA 1.2: Ushairi

**Vipindi** 10

**Umilisi jumuishi:** Mwanafunzi achambue na kutunga aina mbalimbali za mashairi kwa ajili ya mawasiliano, kuelimisha na burudani.

| **Matarajio ya Ujifunzaji**<br>Mwanafunzi aweze: | **Shughuli Pendekezwa za Mafunzo** | **Sampuli ya Tathmini** |
|---|---|---|
| a) kudhihirisha uelewa wa dhana ya ushairi kwa kuzingatia maana, matapo (kimapokeo na huru) na sifa zake bainifu. *(u, v, gs)* | a) Shirikisha wanafunzi katika vikundi au jozi;<br>• Kueleza maana ya ushairi.<br>• Kujadili umuhimu wa ushairi katika jamii.<br><br>b) Ongoza wanafunzi katika vikundi kusikiliza mashairi mbalimbali yaliyorekodiwa kwenye kanda za sauti na kufafanua sifa za ushairi wa Kiswahili.<br><br>c) Husisha wanafunzi katika vikundi kufanya mazoezi ya kukariri mashairi. | a) Angalia wanafunzi wakijadiliana kuhusu maana ya ushairi na umuhimu wake ili kutathmini uwezo wao wa kushirikiana.<br>b) Zungumza na wanafunzi ukiwadadisi kuhusu;<br>• Maana ya ushairi.<br>• Umuhimu wa mashairi katika jamii.<br>• Sifa za ushairi.<br>c) Tathmini;<br>• mawasilisho ya wanafunzi darasani ili kuthibitisha uelewa wao kuhusu;<br>• maana ya ushairi<br>• Sifa za ushairi.<br>• Umuhimu wa mashairi katika jamii. |
| b) kufafanua matumizi ya istilahi za kishairi katika kuchambua mashairi. *(u, s, gs)* | a) Wape wanafunzi katika jozi baadhi ya istilahi za kishairi na kuwaagiza kuzisoma na kueleza maana yake. Waelekeze kuvumbua istilahi nyingine na kuzifafanua.<br><br>b) Katika vikundi au jozi wape wanafunzi mashairi na uwaongoze kuyakariri na kufafanua istilahi mbalimbali zinazotumika katika mashairi husika na kuwasilisha darasani. | a) Angalia na kutathmini ujasiri wa wanafunzi wakieleza maana ya istilahi za kishairi.<br>b) Zungumza na wanafunzi na kuwauliza kudhihirisha uelewa wao wa kina kuhusu matumizi ya istilahi za kishairi.<br>c) Tathmini;<br>• Orodha ya istilahi za kishairi kwa kuzingatia ufafanuzi wa wanafunzi wa istilahi hizo. |

| | | |
|---|---|---|
| c) kulinganisha, na kulinganua mashairi mbalimbali kwa kuzingatia idadi ya mishororo. *(u, v, gs)* | a) Ongoza wanafunzi katika vikundi kufanya utafiti kuhusu aina mbalimbali za mashairi na kuwasilisha matokeo yao darasani.<br><br>b) Wape diwani za mashairi wanafunzi katika vikundi na kuwaongoza kudhihirisha tofauti baina ya mashairi yaliyomo. | a) Angalia wanafunzi wakijadiliana na kubainisha aina za mashairi kwa heshima na kujiamini.<br><br>b) Zungumza na kuuliza wanafunzi kutofautisha mashairi kadhaa kwa kuzingatia idadi ya mishororo.<br><br>c) Tathmini;<br>Kiwango cha ufasaha, uwezo wa kujieleza na ujasiri wa mwanafunzi akiwasilisha kuhusu;<br>• Kutofautisha mashairi kadhaa kwa kurejelea kipengele cha idadi ya mishororo. |

## MADA 1.3: Tamthilia

**Vipindi** 21

**Umilisi jumuishi:** Mwanafunzi achambue, abuni na kuigiza tamthilia mbalimbali kwa ajili ya burudani, kuwasiliana, kuendeleza maadili na kujipatia kipato.

| **Matarajio ya Ujifunzaji**<br>Mwanafunzi aweze: | **Shughuli pendekezwa za Mafunzo** | **Sampuli ya Tathmini** |
|---|---|---|
| a) kudhihirisha uelewa wa dhana ya tamthilia kwa kuzingatia maana na sifa zake katika matini teule. *(u, gs)* | a) Ongoza wanafunzi katika vikundi au jozi;<br>• Kueleza maana ya tamthilia.<br>• Kufafanua sifa za tamthilia.<br>• Kujadili umuhimu wa tamthilia katika jamii na kuwasilisha darasani. | a) Angalia wanafunzi na; kutathmini uwezo wao wa kushirikiana,<br>• kueleza maana ya tamthilia.<br>• kujadili sifa za tamthilia na umuhimu wa tamthilia.<br>b) Zungumza na wanafunzi ukiwadadisi kuthibitisha uelewa wao kuhusu;<br>• sifa za matini za tamthilia.<br>• umuhimu wa tamthilia.<br>c) Tathmini mawasilisho ya wanafunzi kuhusu sifa na umuhimu wa tamthilia katika jamii. |
| b) kubainisha aina mbalimbali za tamthilia na kudhihirisha tofauti zake. *(u, s)* | a) Elekeza wanafunzi katika vikundi au jozi kubunguabongo kuhusu tamthilia walizowahi kusoma na kuwasilisha maoni yao darasani.<br>b) Katika vikundi au jozi, wape wanafunzi matini mbalimbali za tamthilia watambue aina zake na kujadiliana darasani.<br>c) Wanafunzi katika vikundi walinganishe matini za tamthilia na kutambua tofauti zilizopo na kuwasilisha darasani. | a) Angalia wanafunzi na kutathmini uwezo wao wa kushirikiana, kujiamini na kuheshimu maoni ya wenzao wakati wa mjadala.<br>b) Zungumza na wanafunzi ukiwauliza kufafanua;<br>• Aina mbalimbali za tamthilia .<br>• sifa bainifu za tamthilia .<br>c) Tathmini kazi zilizoandikwa na wanafunzi kuhusu<br>• aina na sifa za tamthilia na tofauti zake. |

| | | |
|---|---|---|
| c) kuchambua matumizi ya lugha katika tamthilia kwa kuzingatia *tamathali* za usemi. *(u, v)* | a) Elekeza wanafunzi kusoma tamthilia mbalimbali na kutambua na kufasiri tamathali za usemi katika tamthilia teule.<br><br>b) Ongoza wanafunzi kusoma nakala zilizoteuliwa na kujadili mchango wa kila tamathali katika ukuzaji wa hadithi nzima | a) Angalia wanafunzi wakijadiliana kuhusu tamathali za usemi katika tamthilia teule na kutathmini uwezo wao wa kushirikiana.<br><br>b) Zungumza na wanafunzi ili kuthibitisha uelewa wao kuhusu tamathali za usemi na umuhimu wake katika kuendeleza hadithi.<br><br>c) Tamthmini shughuli za wanafunzi ukizingatia uelewa wao kuhusu matumizi ya tamthali za usemi katika tamthilia teule. |

## Mada 1.4: Riwaya

**Vipindi** 21

**Umilisi jumuishi:** Mwanafunzi achambue na kubuni riwaya mbalimbali kwa ajili ya burudani, kuwasiliana, kukuza maadili na kujikimu kiuchumi.

| **Matarajio ya Ujifunzaji**<br>Mwanafunzi aweze: | **Shughuli pendekezwa za Mafunzo** | **Sampuli ya Tathmini** |
|---|---|---|
| a) kueleza dhana ya riwaya kwa kuzingatia maana na sifa zake. *(u, s, a)* | a) Shirikisha wanafunzi katika vikundi au jozi kubunguabongo kuhusu dhana ya riwaya na kuwasilisha maoni yao darasani.<br>b) Ongoza wanafunzi katika vikundi kufanya utafiti kutoka mtandaoni ama maktabani kuhusu;<br>sifa za riwaya.<br>c) umuhimu wa riwaya katika jamii na kuwasilisha matokeo yao darasani. | a) Angalia wanafunzi katika vikundi wakishirikiana kueleza dhana ya riwaya na utathimini ujasiri wao na uwezo wao wa kujieleza.<br>b) Zungumza na wanafunzi kwa kuwauliza maswali ili kuthibitisha uelewa wao wa;<br>i) Dhana ya riwaya.<br>ii) Sifa za riwaya.<br>iii) Umuhimu wa riwaya katika jamii.<br><br>c) Tathmini mawasilisho ya wanafunzi wakifafanua:<br><br>i) dhana ya riwaya.<br>ii) sifa za riwaya. |

| | | |
|---|---|---|
| | | iii) umuhimu wa riwaya katika jamii. |
| b) kufafanua aina mbalimbali za riwaya kwa kuzingatia tofauti zake. *(k,u,gs)* | a) Katika vikundi au jozi, shirikisha wanafunzi kufanya utafiti kuhusu aina tofauti za riwaya na kutundika matokeo yao darasani.<br>b) Elekeza wanafunzi katika vikundi watafakari juu ya matokeo ya utafiti waliofanya kuhusu aina mbalimbali za riwaya na kuwasilisha darasani.<br>c) Wape wanafunzi matini za riwaya mbalimbali wakiwa katika vikundi na kuwaagiza kufafanua mambo yanayotofautisha riwaya hizo. | a) Angalia na kutathmini uwezo wa wanafunzi wa kushirikiana katika vikundi au jozi kwa heshima wakifanya utafiti kuhusu aina za riwaya.<br>b) Zungumza na wanafunzi kwa kuwadadisi kuhusu:<br>i) uelewa wao wa kina kuhusu aina za riwaya.<br>ii) Tofauti kati ya riwaya mbalimbali.<br>c) Tathmini shughuli za wanafunzi ambazo zinaweza kuwa ama mawasilisho au shughuli za kufafanua kwa maandishi kuhusu:<br>i) aina za riwaya.<br>ii) tofauti za riwaya. |
| c) kuchambua matumizi ya lugha katika riwaya kwa kuzingatia tamathali za usemi. *(u, s, a)* | a) Shirikisha wanafunzi katika vikundi au jozi kufanya utafiti kwa kusoma ama kusikiliza kanda zilizorekodiwa au matini mbalimbali za riwaya ili kutambua tamathali za usemi zilizomo katika riwaya teule.<br>b) Ongoza wanafunzi katika vikundi au jozi kueleza maana ya tamathali za usemi walizotambua katika riwaya teule.<br>c) Elekeza wanafunzi katika vikundi au jozi kujadili umuhimu wa tamathali katika kusawiri ujumbe wa mwandishi wa riwaya. | a) Angalia na kutathmini uwezo wa wanafunzi wa kujieleza, kushirikiana na wenzao na ujasiri wao huku wakichambua matumizi ya tamathali za usemi katika riwaya teule.<br>b) Zungumza na wanafunzi ukiwadadisi ili kugundua uelewa wao kuhusu:<br>i) matumizi ya tamathali za usemi katika riwaya teule.<br>ii) Nafasi ya tamathali za usemi katika kufanikisha ujumbe wa mwandishi wa riwaya teule.<br>c) Tathmini mawasilisho ya wanafunzi kuhusu:<br>i) Uchambuzi wa matumizi ya tamathali za usemi katika riwaya teule.<br>ii) umuhimu wa matumizi ya tamathali za usemi katika riwaya. |

# Kidato Cha Tano Muhula Wa Pili

## MADA 2.1: Nathari

**Vipindi** 18

**Umilisi jumuishi:** Mwanafunzi achanganue na kubuni kazi mbalimbali za nathari kwa kuzingatia vipengele vya kifasihi ili kuimarisha ustadi wa kuandika na mawasiliano bora.

| **Matarajio ya Ujifunzaji** Mwanafunzi aweze: | **Shughuli pendekezwa za Mafunzo** | **Sampuli ya Tathmini** |
|---|---|---|
| a) kuchambua matumizi ya lugha katika kazi za nathari. *(s, gs)* | a) Shirikisha wanafunzi katika jozi au vikundi kusoma matini za nathari na kutambua mbinu za lugha zinazotumika katika matini husika na kuwasilisha darasani.<br>b) Ongoza wanafunzi katika vikundi vidogo, kila kikundi kipewe mbinu tofauti ya lugha ili kuchanganua matumizi yake katika matini husika. Kwa mfano, kikundi fulani kinaweza kupewa jukumu la kuchanganua matumizi ya sitiari na<br>b) kikundi kingine kiangalie tashbihi.<br><br>Kila kikundi kiwasilishe matokeo yake darasani kwa kujadili jinsi mbinu fulani ya lugha inavyofanikisha ujumbe. | a) Angalia na kutathmini uwezo wa wanafunzi wa kusoma matini na kutambua mbinu za lugha zinazotumiwa katika matini teule ya nathari.<br>b) Dadisi wanafunzi kuhusu:<br>i) Maana ya mbinu za lugha teule.<br>ii) matumizi ya mbinu mbalimbali za lugha zilizotumiwa katika nathari teule.<br>c) Tathmini mjadala wa wanafunzi kuhusu:<br>i) maana ya mbinu za lugha walizotambua katika nathari teule.<br>ii) Wanafunzi waandike kazi fupi ya nathari inayosheheni baadhi ya mbinu za lugha walizojifunza. |
| b) kutathmini vipengele vya mtindo katika kazi za nathari kwa kuchambua jinsi mtindo unavyokuza ujumbe na upekee wa kisanii wa matini. *(v,s, gs)* | a) Katika vikundi au jozi, ongoza wanafunzi; kubunguabongo kuhusu dhana ya mtindo kama inavyotumiwa katika kazi za kifasihi.<br>b) Ongoza wanafunzi katika vikundi kusoma kazi mbalimbali za nathari na kutambua vipengele vya mtindo vilivyojitokeza katika matini teule.<br>c) Weka wanafunzi katika vikundi viwili au jozi mbili. | a) Angalia wanafunzi na kutathmini uwezo wao wa kushirikiana katika vikundi kueleza maana ya mtindo na kutambua vipengele vyake katika matini teule.<br>b) Zungumza na wanafunzi kwa kuwauliza maswali ya kuwachochea ili kuthibitisha uelewa wao kuhusu mtindo katika matini teule. |

| | | |
|---|---|---|
| | Wape matini mbili za waandishi tofauti na kuwaongoza kulinganisha mtindo kwa kutambua upekee wa matini hizo kisanii. Wanafunzi wawasilishe matokeo yao darasani.<br>d) Katika jozi au mmojammoja, ongoza wanafunzi kutunga au kusimulia kazi yoyote ya nathari kwa kutumia vipengele anuwai vya mtindo walivyojifunza. | c) Tathmini masimulizi au tungo mbalimbali zilizoandikwa na wanafunzi kuthibitisha ikiwa walielewa dhana ya mtindo na matumizi yake. |

## MADA 2.2: Ushairi

**Vipindi** 18

**Umilisi jumuishi:** Mwanafunzi achambue na kutunga aina mbalimbali za mashairi kwa ajili ya mawasiliano, kuelimisha na burudani.

| **Matarajio ya Ujifunzaji**<br>Mwanafunzi aweze: | **Shughuli Pendekezwa za Mafunzo** | **Sampuli ya Tathmini** |
|---|---|---|
| a) kudhihirisha uelewa wa muundo wa shairi kwa kuzingatia mada, beti, vipande na mizani ya mashairi ya kimapokeo na huru. *(k, u, gs)* | a) Ongoza wanafunzi katika vikundi au jozi:<br>i) kufasili dhana ya muundo wa shairi.<br>ii) Kupambanua baadhi ya vipengele vya muundo wa shairi.<br>iii) Kujadili dhima ya vipengele hivyo vya muundo.<br><br>b) Wape wanafunzi katika vikundi au jozi mashairi mbalimbali kubainisha vipengele husika vya muundo na kuwasilisha darasani. | a) Angalia na kutathmini wanafunzi katika vikundi au jozi wakishirikiana kufasili dhana ya muundo wa shairi. Zingatia ujasiri wao, uwezo wa kujieleza, n.k<br><br>b) Zungumza na wanafunzi ukiwadadisi ili kuthibitisha uelewa wao kuhusu:<br>i) dhana ya muundo wa shairi.<br>ii) namna walivyoweza kupambanua muundo wa kishairi.<br>iii) Uhusiano uliopo baina ya vipengele vya muundo.<br><br>c) Tathmini mawasilisho ya wanafunzi ili kuthibitisha kuhusu uchambuzi wa vipengele husika vya muundo wa shairi. |

| | | |
|---|---|---|
| b) kudhihirisha uelewa wa ujumbe katika mashairi huru na ya kimapokeo. *(v, s)* | a) Ongoza wanafunzi katika vikundi kukariri mashairi teule darasani. Waelekeze kutambua ujumbe katika mashairi waliyokariri.<br><br>b) Elekeza wanafunzi kufanya utafiti katika mashairi ya mtandaoni na kutoka kwenye diwani teule ili kuchambua ujumbe wake. Waongoze kuwasilisha matokeo yao darasani. | a) Angalia na kusikiliza wanafunzi katika vikundi;<br>i) Wakikariri mashairi teule kadhaa.<br>ii) Kujadili ujumbe unaojitokeza katika mashairi teule. Zingatia uwezo wao wa kujieleza, kuheshimiana, n.k<br>b) Zungumza na wanafunzi kwa kuwauliza ili kuthibitisha uwezo/ujuzi wao wa:<br>i) Kukariri mashairi.<br>ii) Kuchambua ujumbe katika mashairi kadhaa.<br>c) Tathmini:<br>i) Uwezo wa wanafunzi wa kukariri mashairi.<br>ii) Umahiri wa wanafunzi wa kuchambua ujumbe katika mashairi teule. |
| c) kuchambua ufundi wa kisanaa katika mashairi kwa kuzingatia taswira, sitiara, tashibihi na tashihisi katika mashairi ya kimapokeo na huru. (*k, u, v, a)* | a) Ongoza wanafunzi katika vikundi/jozi kufasiri dhana ya ufundi wa kisanaa katika mashairi au mbinu za kishairi, kueleza mifano teule na kuwasilisha darasani.<br><br>b) Wape wanafunzi katika jozi mashairi ili kuchambua mbinu za kisanaa zilizotumiwa na mshairi pamoja na uamilifu wake. | a) Angalia wanafunzi wakishirikiana katika:<br>i) kufasiri dhana ya mbinu za kishairi.<br>ii) kuchambua mbinu teule za kishairi kutoka mashairi.<br>b) Zungumza na wanafunzi kwa kuwauliza;<br>i) namna mbinu za kishairi zilivyotumiwa katika mashairi.<br>ii) Jinsi mbinu za kishairi zinavyojenga ujumbe katika shairi.<br>iii) Kwa nini mbinu za kishairi ni muhimu katika shairi.<br>c) Tathmini uchambuzi wa wanafunzi wa;<br>i) mbinu za kishairi katika mashairi teule.<br>ii) Umakinifu wa wanafunzi katika mawasilisho yao. |

## MADA 2.3: Tamthilia

**Vipindi** 36

**Umilisi jumuishi:** Mwanafunzi achambue, abuni na kuigiza tamthilia mbalimbali kwa ajili ya burudani, kuwasiliana, kuendeleza maadili na kujipatia kipato.

| **Matarajio ya Ujifunzaji**<br>Mwanafunzi aweze: | **Shughuli pendekezwa za Mafunzo** | **Sampuli ya Tathmini** |
|---|---|---|
| a) kuchambua vipengele vya tamthilia kwa kuzingatia wahusika, mandhari na ploti. *(u, v, gs)* | a) Ongoza wanafunzi katika vikundi kufanya utafiti kuhusu vipengele vya wahusika, mandhari na ploti na kuwasilisha matokeo yao darasani.<br>b) Wape wanafunzi katika vikundi au jozi tamthilia teule na kuwaelekeza kuchunguza mchango wa mandhari katika ujenzi wa wahusika na ujumbe wa mwandishi. Waagize kuwasilisha matokeo yao darasani.<br>c) Husisha wanafunzi katika vikundi kujadili kipengele cha ploti kwa kurejelea tamthilia teule. (Mwanafunzi anaweza kupewa matini iliyochapishwa ama mchezo uliorekodiwa) | a) Angalia uwezo wa wanafunzi wa kushirikiana kwa heshima na ujasiri wa kujadili:<br>i) Vipengele vya wahusika, mandhari na ploti.<br>ii) Jinsi mchango wa vipengele hivyo husaidia katika kusawiri ujumbe.<br>b) Zungumza na wanafunzi ili kuthibitisha ujuzi wao wa kuchambua;<br>i) Vipengele vya wahusika, mandhari na ploti katika tamthilia teule.<br>ii) Umuhimu wa wahusika katika ujenzi wa ploti.<br>iii) Nafasi ya mandhari katika ujenzi wa wahusika.<br>c) Tathmini mawasilisho darasani ili kupima uelewa wa wanafunzi kuhusu vipengele vya wahusika, ploti na mandhari katika tamthilia teule. |

## MADA 2.4: Riwaya

**Vipindi 36**

**Umilisi jumuishi:** Mwanafunzi achambue na kubuni riwaya mbalimbali kwa ajili ya burudani, kuwasiliana, kukuza maadili na kujikimu kiuchumi.

| **Matarajio ya Ujifunzaji**<br>Mwanafunzi aweze: | **Shughuli Pendekezwa za Mafunzo** | **Sampuli ya Tathmini** |
|---|---|---|
| a) kueleza mbinu za usimulizi katika riwaya. *(s, v, a, gs)* | a) Katika vikundi au jozi ongoza wanafunzi kubunguabongo kuhusu dhana ya mbinu za usimulizi na kuwasilisha matokeo yao darasani.<br><br>b) Elekeza wanafunzi katika vikundi kusikiliza au kusoma matini za riwaya mbalimbali na kujadili mbinu za usimulizi zinazodhihirika katika matini hizo.<br><br>c) Shirikisha wanafunzi katika vikundi kufafanua umuhimu wa mbinu hizo katika kufaniksha ujumbe wa riwaya. | a) Angalia na kutathmini wanafunzi katika vikundi au jozi wakibunguabongo kuhusu dhana ya mbinu za usimulizi katika riwaya teule. Chunguza uwezo wao wa kushirikiana katika vikundi, ujasiri, n.k<br><br>b) Zungumza na kudadisi wanafunzi katika vikundi au binafsi ili kuthibitisha ujuzi wa;<br>i) Kujadili mbinu za kisanii wanazotumia waandishi wa riwaya katika kuwasilisha ujumbe wao katika riwaya teule.<br>ii) Kuchambua umuhimu wa mbinu hizo katika kusawiri ujumbe.<br><br>c) Tathmini mawasilisho ya wanafunzi darasani ili kupima uelewa wao wa mbinu za usimulizi na mchango wake katika kusawiri ujumbe. |
| b) kuchambua maudhui katika riwaya teule. (u, v, a, gs) | a) Shirikisha wanafunzi katika vikundi au jozi kusoma matini teule za riwaya.<br>b) Elekeza wanafunzi katika vikundi kuchanganua maudhui yaliyomo katika riwaya teule. Waagize kuwasilisha kazi zao darasani. | a) Angalia na kutathmini wanafunzi katika vikundi wakisoma matini za riwaya teule. Chunguza uwezo wao wa kusoma na kushirikiana, ujasiri, n.k |

| | | |
|---|---|---|
| | | b) Zungumza na wanafunzi ili:<br>i) Kuthibitisha ikiwa wanasoma riwaya teule kwa makini.<br>ii) Kutambua umahiri wao wa kuchambua maudhui katika riwaya teule.<br>c) Tathimini mawasilisho ya darasani kupima uwezo wa wanafunzi wa kuchanganua maudhui katika riwaya teule. |

## Kidato Cha Tano Muhula Wa Tatu

### MADA 3.1: Nathari

**Vipindi** 18

**Umilisi jumuishi:** Mwanafunzi achanganue na kubuni kazi mbalimbali za nathari kwa kuzingatia vipengele vya kifasihi ili kuimarisha ustadi wa kuandika na mawasiliano bora.

| **Matarajio ya Ujifunzaji**<br>Mwanafunzi aweze: | **Shughuli Pendekezwa za Mafunzo** | **Sampuli ya Tathmini** |
|---|---|---|
| a) kuchambua mitazamo mbalimbali katika kazi za nathari kwa kutathmini jinsi mtazamo teule wa hadithi unavyoathiri uelewa wa msomaji kuhusu hadithi. *(s, v, gs)* | a) Katika jozi au vikundi, ongoza wanafunzi kufanya utafiti kuhusu dhana ya mtazamo na kuwasilisha matokeo yao darasani.<br>b) Wape wanafunzi katika vikundi matini ya kifasihi iliyoandika kwa kutumia mtazamo fulani kama matumizi ya nafsi ya kwanza (ni-), waagize wanafunzi kuandika upya matini hiyo kwa kutumia mtazamo mwingine kama nafsi ya pili au ya tatu. Baadaye, waagize kuwasilisha kazi zao na kueleza namna mabadiliko ya mtazamo yanavyoleta tofauti katika matini. | a) Angalia na kutathmini uwezo wa wanafunzi wa kufanya utafiti, mawasiliano bora na kufanya kazi kwa ushirikiano kueleza dhana ya mtazamo kama inavyotumiwa katika kazi za kifasihi.<br>b) Zungumza na wanafunzi kwa kuwadadisi kuhusu;<br>i) maana ya mtazamo katika kazi za kifasihi.<br>ii) matumizi na dhima ya mtazamo katika kazi mbalimbali za kifasihi. |

| | | |
|---|---|---|
| | c) Ongoza wanafunzi katika vikundi kujadili jinsi usuli na itikadi ya mtu inavyoathiri mtazamo wake kuhusu suala fulani.<br>d) Uliza wanafunzi kueleza namna mtazamo unavyochangia kuelewa sifa za mhusika teule.<br>e) Teua madondoo ya nathari yenye mitazamo tofauti. Waulize wanafunzi kuyalinganisha kwa kuzingatia dhima au athari ya mtazamo katika kazi za kifasihi. Kila kikundi kitawasilisha matokeo yake darasani ama kwa maandishi au masimulizi. | c) Tathmini kazi za wanafunzi walizoandika au kuwasilisha kimasimulizi kuhusu mtazamo. |
| b) kufafanua dhamira ya mwandishi katika kazi za nathari na kufasiri athari yake kwa msomaji.<br>*a. (v, s, gs)* | a) Uliza wanafunzi katika vikundi au jozi kueleza dhana ya dhamira ya mwandishi kama inavyotumiwa katika kazi za kifasihi.<br>b) Ongoza wanafunzi katika vikundi kufanya utafiti kuhusu usuli wa mwandishi fulani, utamaduni wake na historia yake na kueleza namna mambo haya yanavyoakisiwa katika kazi zake.<br>c) Wanafunzi katika vikundi viwili au majozi wajadili dhamira ya matini tofauti na kuwasilisha matokeo yao darasani.<br>d) Katika jozi au mmoja mmoja, wape wanafunzi mada mbalimbali na kuwaongoza kutunga au kusimulia kazi yoyote ya nathari kwa kuzingatia mada hizo. | a) Angalia wanafunzi na kutathmini uwezo wao wa kuwasiliana na kushirikiana katika vikundi kueleza dhamira ya mwandishi.<br>b) Zungumza na wanafunzi kwa kuwauliza maswali ya kuwachochea ili kuthibitisha uelewa wao kuhusu suala la dhamira ya mwandishi katika matini husika.<br>c) Tathmini masimulizi au tungo mbalimbali zilizoandikwa na wanafunzi kuthibitisha ikiwa walielewa dhana ya dhamira ya mwandishi. |

## MADA 3.2: Ushairi

**Vipindi** 18

**Umilisi jumuishi:** Mwanafunzi achambue na kutunga aina mbalimbali za mashairi kwa ajili ya mawasiliano, kuelimisha na burudani.

| **Matarajio ya Ujifunzaji**<br>Mwanafunzi aweze: | **Shughuli Pendekezwa za Mafunzo** | **Sampuli ya Tathmini** |
|---|---|---|
| a) kupambanua bahari za ushairi kwa kuzingatia vigezo vya mpangilio wa vina na urefu wa mishororo. *(k, u, s, a)* | a) Wape wanafunzi katika vikundi mashairi mbalimbali na kuwaongoza;<br>i) kutambua vina na utaratibu wake.<br>ii) kubaini urefu wa mishororo yake.<br>iii) kulinganisha vina na urefu wa mishororo yake.<br><br>b) Elekeza wanafunzi katika vikundi au jozi kukariri au kusikiliza mashairi yaliyorekodiwa na kushirikiana kujadili bahari kulingana na vina vyake.<br><br>c) Wape wanafunzi katika vikundi diwani ya mashairi na kuwaagiza kuainisha mashairi hayo kwa kurejelea vigezo husika. (Kwa wasioweza kusoma, warekodie mashairi ili washiriki katika ujifunzaji.) | a) Angalia na kutathmini wanafunzi katika vikundi au jozi wakishirikiana:<br>i) Kutambua vina vya mashairi.<br>ii) Kujadili bahari za mashairi.<br>iii) Kulinganisha urefu wa mishororo ya mashairi.<br>iv) kusikiliza rekodi za mashairi.<br>b) Zungumza na wanafunzi na kuwauliza kuhusu;<br>i) bahari walizowahi kusikia.<br>ii) fasili ya bahari, vina na mishororo.<br>iii) rekodi waliyoisikia.<br>iv) sifa za bahari walizobaini.<br>c) Tathmini:<br>i) mawasilisho ya wanafunzi darasani kuhusu sifa bainifu za bahari teule.<br>ii) Kupambanua bahari za mashairi kadhaa kwa kutumia vigezo husika. |
| b) kuchanganua bahari za ushairi kwa kuzingatia vigezo vya mpangilio wa vipande na urefu wa shairi. *(k, u, s, a)* | a) Wape wanafunzi katika vikundi diwani teule:<br>i) kutambua vipande katika mashairi.<br>ii) kueleza majina ya vipande hivyo.<br>iii) kulinganisha mashairi kwa kutegemea urefu wake. | a) Angalia wanafunzi wakishirikiana:<br>i) kutambua vipande na majina yake katika mashairi.<br>ii) kujadili bahari za mashairi kulingana na idadi ya vipande pamoja na urefu wa mashairi. |

| | | |
|---|---|---|
| | iv) walinganishe mashairi mbalimbali kwa kutegemea idadi ya vipande.<br><br>b) Ongoza wanafunzi kubunguabongo kuhusu bahari mbalimbali kulingana na vigezo vya urefu wa mashairi pamoja na idadi ya vipande vyake kisha wawasilishe darasani. | iii) Kuwasilisha majibu yao darasani.<br>b) Zungumza na wanafunzi kwa kuwauliza:<br>i) Kueleza maana ya vipande.<br>ii) Kueleza majina ya vipande walivyotambua.<br>c) Tathmini: Umahiri wa wanafunzi wa kuchanganua bahari za ushairi kwa kuzingatia vigezo vya mpangilio wa vipande na urefu wa shairi. |

## MADA 3.3: Tamthilia

**Vipindi** 36

**Umilisi jumuishi:** Mwanafunzi achambue, abuni na kuigiza tamthilia mbalimbali kwa ajili ya burudani, kuwasiliana, kuendeleza maadili na kujipatia kipato.

| **Matarajio ya Ujifunzaji**<br>Mwanafunzi aweze: | **Shughuli pendekezwa za Mafunzo** | **Sampuli ya Tathmini** |
|---|---|---|
| a) kuchanganua mbinu za uigizaji wa tamthilia. *(s ,a ,v gs)* | a) Katika vikundi au jozi ongoza wanafunzi kubunguabongo kuhusu dhana ya mbinu za maigizo yaani mbinu zinazotumiwa kuigiza katika sanaa ya michezo kama vile dayolojia, monolojia, uzungumzaji nafsi, n.k na kuwasilisha matokeo yao darasani.<br>b) Elekeza wanafunzi katika vikundi kusoma matini za tamthilia mbalimbali na kujadili mbinu za uigizaji wa tamthilia zinazodhihirika katika matini hizo na umuhimu wake. | a) Angalia na kutathmini wanafunzi katika vikundi au jozi wakibunguabongo kuhusu dhana ya mbinu za uigizaji wa tamthilia kama inavyotumiwa katika sanaa za maigizo. Chunguza uwezo wao wa kushirikiana katika vikundi, ujasiri, n.k<br>b) Zungumza na kudadisi wanafunzi katika vikundi au binafsi ili kuthibitisha ujuzi wa;<br>c) Kujadili mbinu za uigizaji wa tamthilia zinazotumiwa na waandishi wa tamthilia.<br>d) Kuchambua umuhimu wa mbinu hizo katika kuendeleza mchezo.<br>e) Tathmini mawasilisho ya wanafunzi darasani ili kupima uelewa wao wa |

| | | |
|---|---|---|
| | c) Shirikisha wanafunzi katika vikundi kuandika au/na kuigiza igizo fupi kwa kurejelea matumizi sahihi ya mbinu za uigizaji wa tamthilia teule. | matumizi ya mbinu za uigizaji wa tamthilia na mchango wake katika sanaa za maigizo. |
| b) kuchanganua sifa za maleba na umuhimu wake katika sanaa za maigizo. *(u,s,v, gs)* | a) Ongoza wanafunzi katika vikundi au jozi kufanya utafiti kuhusu dhana ya maleba na kuwasilisha matokeo yao darasani.<br>b) Elekeza wanafunzi katika vikundi kufafanua umuhimu wa maleba katika sanaa za maigizo.<br>c) Shirikisha wanafunzi katika vikundi au binafsi kutengeneza maleba mazuri na kuyatumia kuigiza igizo fulani darasani. | a) Angalia wanafunzi na kutathmini uwezo wao wa kushirikiana katika vikundi kujadili dhana ya maleba kwa kuzingatia sifa za maleba na umuhimu wake.<br>b) Zungumza na wanafunzi ukiwadadisi ili kuthibitisha uelewa wao kuhusu;<br>i) Dhana ya maleba.<br>ii) Sifa za maleba.<br>iii) Jinsi ya kutengeneza maleba.<br>iv) Mambo ya kuzingatia wakati wa kuteua au kutengeneza maleba.<br>v) umuhimu wa maleba.<br>c) Tathmini maleba yaliyotengenezwa au teuliwa wakati wa kuigiza kwa kuzingatia:<br>i) sifa za maleba<br>ii) vigezo vya kuzingatia wakati wa kuteua maleba. |

## MADA 3.4: Riwaya

**Vipindi** 36

**Umilisi jumuishi:** Mwanafunzi achambue na kubuni riwaya mbalimbali kwa ajili ya burudani, kuwasiliana, kukuza maadili na kujikimu kiuchumi.

| **Matarajio ya Ujifunzaji**<br>Mwanafunzi aweze: | **Shughuli Pendekezwa za Mafunzo** | **Sampuli ya Tathmini** |
|---|---|---|
| a) kufafanua dhana ya mgogoro katika riwaya. *(u, v, a, gs)* | a) Katika vikundi ongoza wanafunzi kubunguabongo kuhusu dhana ya mgogoro kama inavyotumiwa katika riwaya na kufanya mawasilisho darasani.<br><br>b) Wape wanafunzi matini mbalimbali za riwaya teule. Waagize kuzisoma na kuchanganua migogoro inayodhihirishwa katika matini hizo na athari ya migogoro hiyo. | a) Angalia wanafunzi katika vikundi na kutathmini ujasiri wao wa kujadiliana kuhusu dhana ya migogoro.<br><br>b) Zungumza na wanafunzi katika vikundi au jozi ukichunguza ushirikiano wao katika kuchambua migogoro inayojitokeza katika riwaya teule na athari yake.<br><br>c) Tathmini kazi za wanafunzi walizowasilisha kuhusu uchambuzi wa mgogoro katika riwaya teule. |
| b) kuchambua maudhui katika riwaya teule (mwendelezo) (s, v, a, gs) | a) Ongoza wanafunzi katika vikundi kufanya utafiti kuhusu vipengele vinavyochambuliwa katika maudhui, kama vile mafunzo, maadili, dhamira, n.k, na kufanya mawasilisho darasani.<br><br>b) Shirikisha wanafunzi katika vikundi au jozi kusoma matini teule za riwaya.<br>c) Elekeza wanafunzi katika vikundi kuchanganua maudhui yaliyo katika riwaya teule. Waagize kuwasilisha kazi zao darasani. | a) Angalia na kutathmini wanafunzi katika vikundi wakifafanua vipengele vinavyochambuliwa katika maudhui. Chunguza uwezo wao wa kujieleza, kushirikiana, ujasiri, n.k<br><br>b) Zungumza na wanafunzi na kuwaagiza:<br>i) Kueleza vipengele tunavyozingatia wakati wa kuchambua maudhui.<br>ii) Kujadili maudhui makuu katika riwaya teule.<br>c) Tathimini mawasilisho ya darasani kupima uwezo wa wanafunzi wa kuchanganua maudhui kwa kina katika riwaya teule. |

# Kidato Cha Sita Muhula Wa Kwanza

## MADA 1.1: Nathari

**Vipindi** 18

**Umilisi jumuishi:** Mwanafunzi achanganue na kubuni kazi mbalimbali za nathari kwa kuzingatia vipengele vya kifasihi ili kuimarisha ustadi wa kuandika na mawasiliano bora.

| **Matarajio ya Kujifunza**<br>Mwanafunzi aweze: | **Shughuli Pendekezwa za Mafunzo** | **Sampuli ya Tathmini** |
|---|---|---|
| a) kujadili mbinu mbalimbali za uandishi wa kazi za nathari, kama vile mazungumzo, maelezo na mtazamo. *(u, v, a)* | a) Katika vikundi, elekeza wanafunzi kubunguabongo kuhusu vipengele muhimu katika utunzi wa kazi za nathari na kufanya mawasilisho darasani.<br>b) Agiza wanafunzi kusoma kazi mbalimbali za nathari, zikiwemo hadithi fupi, riwaya, novela na insha. Waelekeze wanafunzi kujadili mbinu za uandishi zinazotumiwa na waandishi tofauti wa kazi walizosoma.<br>c) Weka wanafunzi katika vikundi viwili, kila kikundi kipewe matini tofauti ya nathari na kuagizwa kutambua namna waandishi walivyojenga hadithi na wahusika wao katika matini husika na kufanya mawasilisho darasani. | a) Angalia wanafunzi wakibunguabongo kuhusu vipengele vya ubunifu wa kazi za nathari na kutathmini umahiri wao wa kushirikiana katika vikundi na kujieleza kwa ujasiri.<br>b) Zungumza na wanafunzi ukiwadadisi kuhusu;<br>i) mbinu mbalimbali za uandishi wa kazi za nathari.<br>ii) jinsi waandishi wanavyobuni hadithi zao.<br>c) Tathmini mawasilisho ya wanafunzi na kazi zao andishi ukizingatia:<br>i) mbinu za uandishi wa kazi za nathari.<br>ii) ujenzi wa wahusika katika kazi za nathari. |
| b) kuunda na kusimulia kazi asilia za nathari, kutumia mbinu mbalimbali za usimulizi na vipengele vya kisanii ili kuwasilisha kwa ufanisi maudhui, kujenga wahusika na kumvutia msomaji. *(s, v, a,gs)* | a) Katika jozi, shirikisha wanafunzi; kufanya mpangokazi wa kazi ya nathari wanayotaka kuandika na kuwasilisha maoni yao darasani.<br>b) Ongoza wanafunzi kuandika muhtasari wa kazi zao kwa kuzingatia vipengele vikuu vya ploti.<br>c) Ongoza wanafunzi kutunga au kusimulia kazi za nathari walizotunga wanafunzi. | a) Angalia wanafunzi na kutathmini ustadi wao wa kujieleza na kushirikiana katika vikundi kufanya kiunzi cha kazi.<br>b) Uliza wanafunzi maswali ya kuchochea kuthibitisha kuwa kazi zao zina mtiririko.<br>c) Tathmini masimulizi au kazi walizotunga wanafunzi kwa kuzingatia: mbinu za uandishi wa kazi wa nathari |

## MADA 1.2: Ushairi

**Vipindi** 18

**Umilisi jumuishi:** Mwanafunzi achanganue, atunge na kuchapisha mashairi mbalimbali kwa ajili ya kuburudisha, kukuza maadili, kuwasiliana na kujipatia kipato.

| **Matarajio ya Ujifunzaji**<br>Mwanafunzi aweze: | **Shughuli Pendekezwa za Mafunzo** | **Sampuli ya Tathmini** |
|---|---|---|
| a) kutunga aina mbalimbali za mashairi asilia kwa kutumia mbinu anuwai za kishairi kudhihirisha ubunifu na uelewa wa miundo ya kishairi. *(u, s, a)* | a) Ongoza wanafunzi katika vikundi:<br>i) Kubunguabongo kuhusu mambo ya kuzingatia wakati wa kuteua mada ya kutungia shairi na kuwasilisha maoni yao darasani.<br>ii) Kueleza hali mbalimbali zinazoweza kumchochea mtu kutunga shairi.<br>iii) Kufafanua hatua zinazochukuliwa wakati wa kutunga shairi.<br>iv) Kujadili vipengele vya uhuru wa mshairi.<br>b) Katika vikundi au jozi wape wanafunzi mada mbalimbali zinazosheheni hali anuwai kama hali ya huzuni, furaha, mapenzi, hofu, n,k na kuwaongoza kutunga mashairi.<br>c) Shirikisha wanafunzi katika vikundi au jozi kuwasilisha mashairi waliyotunga darasani. | a) Angalia na kutathmini wanafunzi katika vikundi au jozi wakishirikiana:<br>i) Kujadili mambo yanayozingatiwa wakati wa kutunga mashairi.<br>ii) Kueleza hali mbalimbali zinazoweza kumchochea mtu kutunga shairi.<br>iii) Kufafanua hatua zinazochukuliwa wakati wa kutunga shairi.<br>iv) Kueleza vipengele vya uhuru wa mshairi.<br>b) Zungumza na wanafunzi na kuwauliza kuhusu:<br>i) mambo ya kuzingatiwa wakati wa kutunga shairi.<br>ii) Hali mbalimbali zinazoweza kumchochea mtu kutunga shairi.<br>iii) Hatua za kuchukua wakati wa kutunga shairi.<br>c) Tathmini: Uwasilishaji wa mashairi yaliyotungwa na wanafunzi darasani kwa kuzingatia vipengele vya muundo wa shairi. |

## MADA 1.3: Tamthilia

**Vipindi** 36

**Umilisi jumuishi:** Mwanafunzi achambue, abuni na kuchapisha tamthilia mbalimbali pamoja na kuigiza tamthilia anuwai kwa azma ya kuburudisha, kuendeleza maadili na kujipatia kipato.

| **Matarajio ya Ujifunzaji** Mwanafunzi aweze: | **Shughuli Pendekezwa za Mafunzo** | **Sampuli ya Tathmini** |
|---|---|---|
| a) kujadili mgogoro katika tamthilia na umuhimu wake katika uendelezaji wa hadithi nzima. *(u, gs,v,a)* | a) Katika vikundi ongoza wanafunzi kubunguabongo kuhusu dhana ya mgogoro kama inavyotumiwa katika tamthilia na kufanya mawasilisho darasani.<br><br>b) Wape wanafunzi matini mbalimbali za tamthilia teule. Waagize kuzisoma na kuchanganua migogoro inayodhihirishwa katika matini hizo na athari ya migogoro hiyo. | a) Angalia wanafunzi katika vikundi na kutathmini ujasiri wao wa kujadiliana kuhusu dhana ya migogoro.<br>b) Zungumza na wanafunzi katika vikundi au jozi ukichunguza ushirikiano wao katika kuchambua migogoro inayojitokeza katika tamthilia teule na athari yake.<br>c) Tathmini kazi za wanafunzi walizowasilisha kuhusu uchambuzi wa mgogoro katika tamthilia teule. |
| b) kupambanua dhima ya maelekezo ya jukwaa katika michezo ya kuigiza. *(u, gs,v,a)* | a) Ongoza wanafunzi katika vikundi au jozi kubunguabongo kuhusu dhana ya maelekezo ya jukwaa na kuwasilisha maoni yao darasani.<br><br>b) Elekeza wanafunzi katika vikundi kujadili umuhimu wa maelekezo ya jukwaa katika tasnia ya sanaa za maigizo.<br><br>*(Rejelea maelekezo ya jukwaa katika tamthilia teule)*<br><br>c) Shirikisha wanafunzi katika vikundi au jozi kuandika maelekezo ya jukwaa ya igizo husika. | a) Angalia na kutathmini wanafunzi wakibunguabongo kuhusu dhana ya maelekezo ya jukwaa. Zingatia uwezo wao wa kujieleza, kushirikiana, kuheshiana, n.k<br>b) Zungumza na wanafunzi na kuwaagiza kufafanua maelekezo ya jukwaa katika tamthilia teule na kueleza umuhimu wa maelekezo ya jukwaa.<br>c) Tathmini:<br>i) Umahiri wa wanafunzi wa kujadili maelekezo ya jukwaa na umuhimu wake.<br>ii) Shughuli ya wanafunzi ya kuandika maelekezo ya jukwaa kwa ajili ya mchezo fulani wa kuigiza. |

## MADA 1.4: Riwaya

**Vipindi 36**

**Umilisi jumuishi:** Mwanafunzi achambue na kubuni riwaya mbalimbali kwa ajili ya burudani, kuwasiliana, kukuza maadili na kujikimu kiuchumi.

| **Matarajio ya Ujifunzaji**<br>Mwanafunzi aweze: | **Shughuli Pendekezwa za Mafunzo** | **Sampuli ya Tathmini** |
|---|---|---|
| a) kuandika sura za riwaya ili kudhihirisha uelewa wa mbinu za usimulizi, ujenzi wa wahusika na maudhui. (u, gs,v, a) | a) Katika vikundi au jozi ongoza wanafunzi kubunguabongo kuhusu<br>b) vipengele muhimu katika utunzi wa riwaya na kufanya mawasilisho darasani.<br><br>c) Katika jozi, shirikisha wanafunzi kufanya mpangokazi wa sura ya riwaya wanayotaka kuandika na kuwasilisha maoni yao darasani.<br><br>d) Ongoza wanafunzi kuandika muhtasari wa kazi zao kwa kuzingatia vipengele vikuu vya ploti.<br><br>e) Elekeza wanafunzi kutunga kazi kwa kurejelea mpangokazi walioweka. Waagize kutundika kazi zao ukutani. | a) Angalia wanafunzi na kutathmini ustadi wao wa kujieleza na kushirikiana katika vikundi kufanya kiunzi cha kazi.<br><br>b) Dadisi wanafunzi kwa kuwauliza maswali ya kuchochea kuthibitisha kuwa kazi zao zina mtiririko.<br><br>c) Tathmini masimulizi au kazi walizotunga wanafunzi kwa kuzingatia:<br>i) mbinu za uandishi wa riwaya.<br>ii) ujenzi wa wahusika<br>iii) maudhui<br>iv) matumizi ya lugha |

# Kidato Cha Sita Muhula Wa Pili

## MADA 2.1: Nathari

**Vipindi** 18

**Umilisi jumuishi:** Mwanafunzi achanganue na kubuni kazi mbalimbali za nathari kwa kuzingatia vipengele vya kifasihi ili kuimarisha ustadi wa kuandika na mawasiliano bora.

| **Matarajio ya Ujifunzaji** Mwanafunzi aweze: | **Shughuli Pendekezwa za Mafunzo** | **Sampuli ya Tathmini** |
|---|---|---|
| a) kutathmini matumizi ya lugha katika kazi za nathari kwa kuchambua jinsi inavyosaidia kujenga ujumbe wa matini. *(u, s, gs)* | a) Katika vikundi, ongoza wanafunzi kujadili kipengele cha matumizi ya lugha kama kinavyojitokeza katika kazi za nathari na kuwasilisha maoni yao darasani.<br><br>b) Wape wanafunzi matini mbalimbali za nathari na kuwaelekeza kuzisoma na kutambua tamathali za usemi na mbinu nyingine za sanaa zinazojitokeza katika matini husika na kufanya mawasilisho.<br><br>c) Weka wanafunzi katika vikundi au jozi tofauti, kila kikundi kipewe matini tofauti ya nathari na kuongozwa kuiandika upya matini husika kwa kutumia tamathali za usemi tofauti na zile zilizokuwa zimetumiwa awali.<br><br>d) Ongoza wanafunzi katika vikundi au jozi kuandika kazi yoyote ya nathari kwa kudhihirisha matumizi bora ya tamathali za usemi na mbinu nyingine za sanaa. | a) Angalia wanafunzi wakijadiliana kuhusu kipengele cha matumizi ya lugha kutathmini ustadi wao wa kujieleza kwa ujasiri.<br><br>b) Zungumza na wanafunzi ukiwadadisi kuhusu:<br>i) maana ya tamathali za usemi anuwai.<br>ii) matumizi ya tamathali za usemi mbalimbali zinazotumika katika kazi za nathari.<br><br>c) Tathmini kazi za wanafunzi kwa kuzingatia:<br>i) maana ya tamathali ya usemi.<br>ii) matumizi ya tamathali za usemi na mbinu nyingine za sanaa katika matini. |

## MADA 2.2: Ushairi

**Vipindi** 18

**Umilisi jumuishi:** Mwanafunzi achanganue, atunge na kuchapisha mashairi mbalimbali kwa ajili ya kuburudisha, kukuza maadili, kuwasiliana na kujipatia kipato.

| **Matarajio ya Ujifunzaji**<br>Mwanafunzi aweze: | **Shughuli Pendekezwa za Mafunzo** | **Sampuli ya Tathmini** |
|---|---|---|
| a) kuchambua hali, hisia na toni katika mashairi mbalimbali, kuelewa jinsi vipengele hivi vinavyoibua ujumbe katika mashairi. *(u,s,v)* | a) Ongoza wanafunzi katika vikundi au jozi: kufasiri dhana za hali, hisia na toni kama zinavyotumiwa katika kazi za kifasihi.<br>b) Wape wanafunzi katika vikundi au jozi mashairi mbalimbali yanayodhihirisha hali, hisia na toni mbalimbali. Elekeza wanafunzi kutambua vipengele hivi katika mashairi hayo na kuwasilisha kazi zao darasani.<br>c) Wape wanafunzi mada mbalimbali na washirikishe kutunga mashairi yanayodhihirisha hali, hisia na toni mbalimbali. | a) Angalia wanafunzi katika vikundi au jozi wakishirikiana kufasiri dhana za hali, hisia na toni kama zinavyotumika katika mashairi.<br>b) Zungumza na wanafunzi ukiwadadisi kuhusu;<br>• Dhana ya hali katika mashairi.<br>• Dhana ya hisia katika mashairi.<br>• Dhana ya toni katika mashairi.<br>c) Tathmini kazi za wanafunzi kwa kuzingatia uchanganuzi wa dhana za hali, hisia na toni katika mashairi teule. |
| b) kupambanua sauti ya mzungumzaji katika mashairi mbalimbali, kwa kudhihirisha jinsi washairi wanavyotumia kipengele hiki kuwasilisha wahusika na ujumbe katika mashairi. *(u,v,s)* | a) Katika vikundi, elekeza wanafunzi kubunguabongo kuhusu dhana ya sauti ya mzungumzaji kama inavyotumiwa katika mashairi.<br>b) Wape wanafunzi mashairi katika vikundi mbalimbali. Waelekeze kuchunguza namna mwandishi anavyotumia lugha kudhihirisha sauti ya mzungumzaji katika mashairi teule na wawasilishe maoni yao darasani. | a) Angalia na kutathmini wanafunzi katika vikundi:<br>i) Wakibunguabongo kuhusu dhana ya sauti ya mzungumzaji katika mashairi.<br>ii) Wakishirikiana katika vikundi kujifunza.<br>b) Zungumza na wanafunzi kwa kuwauliza:<br>i) Maoni yao kuhusu dhana ya sauti ya mzungumzaji katika mashairi. |

| | | |
|---|---|---|
| | c) Uliza wanafunzi kuchagua ama mtu mashuhuri wanayemjua, mhusika wa kubuni au mtu yeyote wanayemjua na kuandika shairi kwa kurejelea mtazamo wa mtu huyo. | ii) kutambua sauti ya mzungumzaji katika mashairi mbalimbali.<br><br>c) Tathmini kazi za wanafunzi kwa kuzingatia namna mtazamo wa mtu waliyetumia katika mashairi yao unavyoathiri sauti yake. |

## MADA 2.3: Tamthilia

**Vipindi** 36

**Umilisi jumuishi:** Mwanafunzi achambue, abuni na kuchapisha tamthilia mbalimbali pamoja na kuigiza tamthilia anuwai kwa azma ya kuburudisha, kuendeleza maadili na kujipatia kipato.

| **Matarajio ya Ujifunzaji**<br>Mwanafunzi aweze: | **Shughuli Pendekezwa za Mafunzo** | **Sampuli ya Tathmini** |
|---|---|---|
| a) kutunga na kuigiza maonyesho ya tamthilia kwa kuzingatia muundo sahihi. *(k, u,v,a, gs)* | a) Ongoza wanafunzi katika vikundi au jozi kubunguabongo kuhusu vigezo muhimu vinavyozingatiwa wakati wa utunzi wa tamthilia na kuwasilisha maoni yao darasani.<br><br>b) Katika vikundi au jozi, ongoza wanafunzi kutunga onyesho au sehemu moja ya tamthilia na kuwaelekeza kubadilishana miswada yao na kuihariri darasani.<br><br>c) Ongoza wanafunzi katika vikundi kuigiza maonyesho au sehemu za tamthilia walizotunga. | a) Angalia wanafunzi na kutathmini uwezo wao wa kushirikiana, kujiamini na kuheshimu maoni ya wenzao wakati wa mjadala.<br><br>b) Zungumza na wanafunzi ukiwauliza kuhusu;<br>i) Kueleza vigezo vya kuzingatia wakati wa kuandika tamthilia.<br>ii) Kuandika onyesho moja au sehemu moja ya tamthilia.<br><br>c) Tathmini:<br>i) Maonyesho ya tamthilia yaliyotungwa.<br>ii) Maigizo ya wanafunzi. |

## MADA 2.4: Riwaya

**Vipindi** 36

**Umilisi jumuishi:** Mwanafunzi achambue na kubuni riwaya mbalimbali kwa ajili ya burudani, kuwasiliana, kukuza maadili na kujikimu kiuchumi.

| **Matarajio ya Ujifunzaji**<br>Mwanafunzi aweze: | **Shughuli Pendekezwa za Mafunzo** | **Sampuli ya Tathmini** |
|---|---|---|
| a) kuchanganua dhima ya mandhari katika riwaya, kuelewa jinsi mandhari yanavyoathiri ploti, ujenzi wa wahusika na maudhui. *(u, gs, v, a)* | a) Katika vikundi au jozi, ongoza wanafunzi kubunguabongo kuhusu:<br>• Dhana ya mandhari na umuhimu wake katika ujenzi wa wahusika, maudhui na hadithi.<br><br>b) Wape wanafunzi madondoo ya riwaya na kuwaelekeza kuyasoma na kujadili mandhari yanayojitokeza na kupambanua dhima yake katika ujenzi wa maudhui na wahusika wanaoendeleza ploti. | a) Angalia na kutathmini uwezo wa wanafunzi wa kushirikiana katika vikundi, kuheshimiana, n.k. wakati wakibunguabongo kuhusu dhana ya mandhari.<br>b) Zungumza na kudadisi wanafunzi ili kuthibitisha;<br>• uelewa wao wa kipengele cha mandhari.<br>• Dhima ya mandhari katika ujenzi wa wahusika na maudhui.<br>c) Tathmini mawasilisho ya wanafunzi darasani wakichanganua mandhari anuwai katika riwaya teule na mchango wake. |
| b) kuchambua ploti ya riwaya teule, kuelewa vipengele vya ploti kama vile mwanzo/ chanzo cha mgogoro, kukua kwa mgogoro, kilele, mshuko na utatuzi wa mgogoro. *(u, gs, v, a)* | a) Ongoza wanafunzi katika vikundi au jozi: Kufasiri kipengele cha ploti.<br><br>b) Elekeza wanafunzi katika vikundi au jozi kusoma riwaya teule na kupambanua vipengele vya ploti na kuwasilisha darasani. | a) Angalia na kutathmini uwezo wa wanafunzi wa kushirikiana katika vikundi ili kufasiri kipengele cha ploti.<br>b) Zungumza na wanafunzi ukiwashirikisha kufasiri ploti na kufafanua vipengele vyake.<br>c) Tathmini kazi za wanafunzi kuhusu uchambuzi wa ploti katika riwaya teule. |

# Kidato Cha Sita Muhula Wa Tatu

## MADA 3.1: Nathari

**Vipindi** 10

**Umilisi jumuishi:** Mwanafunzi achanganue na kubuni kazi mbalimbali za nathari kwa kuzingatia vipengele vya kifasihi ili kuimarisha ustadi wa kuandika na mawasiliano bora.

| **Matarajio ya Ujifunzaji**<br>Mwanafunzi aweze: | **Shughuli Pendekezwa za Mafunzo** | **Sampuli ya Tathmini** |
|---|---|---|
| a) kuchambua kazi za nathari. *(s, v,a,gs)* | a) Katika vikundi, ongoza wanafunzi kubunguabongo kuhusu vipengele mbalimbali vinavyozingatiwa katika uchambuzi wa kazi za nathari na kufanya mawasilisho darasani.<br><br>b) Mpe kila mwanafunzi katika kikundi au jozi matini yake ya nathari, aisome. Kila jozi ipewe kipengele kimoja cha uchambuzi. Waelekeze kuchambua na kufanya mawasilisho baadaye.<br><br>c) Ongoza wanafunzi kubadilishana kazi zao na kuulizana maswali kuhusu uchambuzi wa kazi mbalimbali za nathari. | a) Angalia wanafunzi wakibunguabongo kuhusu vipengele vinavyozingatiwa katika uchambuzi wa kazi za nathari na kutathmini ustadi wao wa kujieleza kwa ujasiri na kushirikiana katika vikundi<br><br>b) Zungumza na wanafunzi ukiwadadisi kuhusu;<br><br>c) Vipengele mbalimbali vya uchambuzi wa nathari ili kuthibitisha uelewa wao wa vipengele hivyo.<br><br>d) Tathmini mawasilisho ya wanafunzi pamoja na kazi zao nyingine kwa kuzingatia; Vipengele vya uchambuzi wa kazi za nathari. |

## MADA 3.2: Ushairi

**Vipindi** 11

**Umilisi jumuishi:** Mwanafunzi achanganue, atunge na kuchapisha mashairi mbalimbali kwa ajili ya kuburudisha, kukuza maadili, kuwasiliana na kujipatia kipato.

| **Matarajio ya Ujifunzaji**<br>Mwanafunzi aweze: | **Shughuli Pendekezwa za Mafunzo** | **Sampuli ya Tathmini** |
|---|---|---|
| a) kufanya uchambuzi wa kina wa mashairi, kufasiri maudhui, mafunzo na matumizi ya lugha na kueleza jinsi vipengele hivi vinavyochangia kusawiri ujumbe wa shairi. *(u, s, a)* | a) Shirikisha wanafunzi katika vikundi kujadiliana kuhusu vipengele vinavyozingatiwa katika uchambuzi wa mashairi na kuwasilisha maoni yao darasani.<br><br>b) Wape wanafunzi katika vikundi au jozi mashairi na kuwaelekeza kuyakariri au kuyasikiliza yaliyorekodiwa na kushirikiana kutambua vipengele muhimu vya uchambuzi wa mashairi.<br><br>c) Wape wanafunzi katika vikundi kipengele teule cha uchambuzi. Waelekeze kuchambua kwa kina kipengele hicho kwa kutumia shairi au mashairi teule na kufanya mawasilisho darasani.<br><br>d) Wape wanafunzi katika jozi au vikundi mashairi mawili tofauti na kuwaelekeza kufanya uchambuzi linganishi wa mashairi hayo kwa kurejelea vipengele vya uchambuzi wa mashairi na kufanya mawasilisho darasani. | a) Angalia na kutathmini wanafunzi katika vikundi au jozi wakishirikiana:<br>i) Kujadili vipengele vinavyozingatiwa wakati wa kuchambua mashairi.<br>ii) Kuchambua mashairi kadhaa kwa kurejelea vipengele teule.<br><br>b) Zungumza na wanafunzi na kuwauliza maswali ili kutambua uelewa wao kuhusu;<br>i) Vipengele vinavyozingatiwa wakati wa kuchambua mashairi.<br>ii) Washirikishe kuchambua kwa kina mashairi kadhaa ya Kiswahili ili kuthibitisha uelewa wao.<br><br>c) Tathmini: Mawasilisho ya wanafunzi darasani kuhusu vipengele vya uchambuzi wa mashairi. |

## MADA 3.3: Tamthilia

**Vipindi** 21

**Umilisi jumuishi:** Mwanafunzi achambue, abuni na kuchapisha tamthilia mbalimbali pamoja na kuigiza tamthilia anuwai kwa azma ya kuburudisha, kuendeleza maadili na kujipatia kipato.

| **Matarajio ya Ujifunzaji**<br>Mwanafunzi aweze: | **Shughuli Pendekezwa za Mafunzo** | **Sampuli ya Tathmini** |
|---|---|---|
| a) kuchambua kwa kina vipengele vya tamthilia kwa kuzingatia jinsi vinavyoibua ujumbe. *(s v, gs)* | a) Ongoza wanafunzi katika vikundi au jozi<br>i) Kubunguabongo kuhusu vipengele vikuu vya uchambuzi wa tamthilia, k.v maudhui, matumizi ya lugha, n.k<br>ii) kusoma tamthilia teule.<br><br>b) Wape wanafunzi katika vikundi au jozi tamthilia mbalimbali na kuwaelekeza kujadili na kufafanua vipengele husika vya uchambuzi wa tamthilia.<br><br>c) Ongoza wanafunzi katika vikundi kujadili namna tamthilia teule inavyoakisi hali halisi katika jamii. | a) Angalia na kutathmini wanafunzi wakishirikiana kwa heshima na kujiamini wakati wa kubunguabongo: kuhusu vipengele vya uchambuzi wa tamthilia.<br>b) Zungumza na wanafunzi ukiwauliza:<br>i) kujadili vipengele vikuu vya uchambuzi wa tamthilia husika.<br>ii) Kufafanua jinsi tamthilia teule inavyoakisi hali halisi katika jamii zao.<br><br>c) Tathmini shughuli za wanafunzi ili kupima uelewa wa wanafunzi kuhusu vipengele vikuu vya uchambuzi wa tamthilia. |

## MADA 3.4: Riwaya

**Vipindi** 21

**Umilisi jumuishi:** Mwanafunzi achambue na kubuni riwaya mbalimbali kwa ajili ya burudani, kuwasiliana, kukuza maadili na kujikimu kiuchumi.

| **Matarajio ya Ujifunzaji**<br>Mwanafunzi aweze: | **Shughuli Pendekezwa za Mafunzo** | **Sampuli ya Tathmini** |
|---|---|---|
| a) kuchanganua vipengele vya riwaya teule. *(u, gs, v, a)* | a) Katika vikundi au jozi, ongoza wanafunzi kubunguabongo kuhusu vipengele:<br>i) maudhui<br>ii) ploti<br>iii) wahusika<br>iv) mandhari<br>v) matumizi ya lugha au mbinu za sanaa<br><br>b) Shirikisha wanafunzi katika vikundi kusoma matini za riwaya mbalimbali na kuchambua vipengele vilivyotajwa hapo juu katika (a) na kufanya mawasilisho darasani.<br><br>c) Elekeza wanafunzi katika vikundi au jozi kuchambua riwaya teule na kufafanua jinsi inavyoakisi hali halisi katika jamii. | a) Angalia wanafunzi katika vikundi au jozi wakishirikiana kwa kuheshimiana:<br>i) kujadili maudhui katika riwaya teule<br>ii) kufafanua ploti ya riwaya teule.<br>iii) kueleza sifa za wahusika mbalimbali katika riwaya teule.<br>iv) Kupambanua mandhari ya riwaya teule.<br>v) Kuchambua matumizi ya lugha katika riwaya teule.<br><br>b) Zungumza na wanafunzi ukiwashirikisha;<br>i) kujadili maudhui katika riwaya teule<br>ii) kufafanua ploti ya riwaya teule.<br>iii) kueleza sifa za wahusika mbalimbali katika riwaya teule.<br>iv) Kupambanua mandhari ya riwaya teule.<br>v) Kuchambua<br>vi) matumizi ya lugha katika riwaya teule.<br><br>c) Tathmini mawasilisho ya wanafunzi darasani ili kupima uelewa wao wa vipengele vilivyotajwa hapo juu. |

# 3.0 TATHMINI YA FASIHI YA KISWAHILI

## 3.1 Kutathmini Matarajio mapya ya Ujifunzaji

Mtaala huu mpya umeibuka na matarajio mapya ya ujifunzaji. Hii imetokana na kuhamishwa kwa mtaala huu kutoka mkabala wa malengo hadi mkabala wa matarajio ya ujifunzaji unaolenga matumizi ya ujuzi na ujifunzaji wa kina ambao humwongoza mwanafunzi kupata stadi faafu. Aidha, matarajio haya ya ujifunzaji huhitaji mkabala tofauti wa utathmini. Matarajio ya ujifunzaji yaliyomo katika mtaala huu yamepangwa kulingana na viwango vya; ujuzi, ufahamu, stadi, maadili na mitazamo (UUSMM). Hata hivyo, katika mtaala huu, viwango hivi vimerejelewa kwa kutumia akronimu (KUSVA), yaani; ***K-K****nowledge,* ***U-U****nderstanding,* ***S-S****kills,* ***V-V****alues and* ***A-A****ttitudes.* Stadi za msingi pia zinafaa kuangaziwa katika kila shughuli ya funzo kwa ajili ya kutimiza matarajio ya kila funzo. Hata hivyo, katika mtaala huu, akronimu (gs) kwa maana ya stadi msingi *(generic skill)* imetumika.

Si rahisi kutathmini kiwango cha kujifunza maadili na mitazamo kwa njia sawa na kiwango cha ujuzi, ufahamu au stadi kwa sababu hivi vya mwisho ni vya kibinafsi na hubadilikabadilika na hutimizwa baada ya muda mrefu. Hata hivyo, hii haimaanishi kwamba maadili na mitazamo si muhimu au haviwezi kutathminiwa. Hivi pia vinaweza kutathminiwa ingawa si rahisi kama ujuzi, ufahamu na stadi ambavyo vinatathminiwa kupitia kwa mijarabu na mitihani. Maadili na mitazamo vinaweza kutathiminiwa baada ya muda kupitia kuchunguza na kushirikiana na mwanafunzi.

Kwa hiyo, sehemu hii ya ushauri/maelekezo inalenga ujuzi, ufahamu na stadi. Kila kiwango miongoni mwa hivi kina athari zake kwa ujifunzaji na utathmini.

Kutathmini ujuzi na matumizi yake, ufahamu na stadi, tunafaa kuchunguza vitu mbalimbali. Ujuzi unaweza kutathminiwa kupitia mijarabu andishi lakini utathmini wa stadi, matumizi ya yale aliyojifunza mwanafunzi na ufahamu wa kina huhitaji mikabala tofauti. Kwa sababu hii, dhima ya mwalimu katika utathmini ni muhimu sana.

## 3.2 Mitihani

Kutakuwa na mtihani mmoja mwishoni mwa mwaka. Hakutakuwa na mitihani mingine wala mijarabu ambayo itatungwa mwanzoni au mwishoni mwa muhula. Badala yake, kutakuwa na tathmini ya jumla ambayo itajumuisha tathmini endelevu za mwalimu darasani anapofundisha na tathmini hii itajitokeza katika muktadha wa tathmini ya shughuli jumuishi. Wanafunzi pia watatathiminiwa mwishoni mwa ngazi ili kupewa vyeti. Taarifa zaidi kuhusu tathmini ya mwisho wa ngazi zimetolewa katika mwongozo wa tathmini.

## 3.3 Tathmini Endelevu


Katika mtaala huu mpya, dhima ya mwalimu katika utathmini si kutunga mijarabu kwa wanafunzi bali ni kufanya uamuzi wa kitaaluma juu ya ujifunzaji wa wanafunzi katika mchakato wa kawaida wa ufundishaji na ujifunzaji. Uamuzi wa kitaaluma unahusu kiasi ambacho mwanafunzi ametimiza kuhusu matarajio ya ujifunzaji ambayo yamewekwa katika silabasi hii.

Kufanya uamuzi huu, mwalimu anahitajika kuchunguza uzuri wa maendeleo ya wanafunzi katika matarajio yote ya ujifunzaji.

Utathmini endelevu hutokea katika maumbo matatu. Unaweza kufanyika kupitia:

i) **Uchunguzi (Angalia)** – Kuchunguza wanafunzi wakifanya jambo (mbinu hii ni nzuri ya kutathmini stadi kama za kusikiliza na kuongea, maadili na mitazamo ya wanafunzi)
ii) **Uzungumzaji** – Kuuliza wanafunzi maswali na kuongea nao ukiwadadisi (Ni mbinu nzuri ya kutathmini ujuzi na ufahamu wa wanafunzi)
iii) **Matokeo** – Kutathmini juhudi za wanafunzi kupitia kazi walizofanya (maandiko, maigizo, ripoti, tafsiri, uwasilishaji, ramani, michoro, picha, upakaji rangi, nyimbo n.k.), Katika muktadha huu, matokeo yanaangaliwa kama kitu kinachoonekana.

Vipengele hivi vitatu vikitumiwa vyote, taarifa kutoka mojawapo inaweza kupimwa dhidi ya ile ya vipengele vingine viwili (kwa mfano, ushahidi kutoka uchunguzi unaweza kupimwa dhidi ya ushahidi kutoka uzungumzaji na matokeo. Kwa kawaida, hii hurejelewa kama upembetatu *(triangulation)* kama inavyooneshwa katika kielelezo cha hapa chini:




## 3.4 Stadi za Msingi

Stadi za msingi zimejengeka katika silabasi hii na ni sehemu ya matarajio ya ujifunzaji. Kwa hiyo, si muhimu kuzitathmini kivyake. Aidha, zinatathminiwa kama sehemu ya matarajio ya ujifunzaji katika somo husika.

## 3.5 Maadili/ Mitazamo

Si rahisi kutathmini maadili na mitazamo kwa njia sawa na ujuzi, ufahamu na stadi kwa kuwa viwango hivi huwa vya kibinafsi na hubadilikabadilika na hutimizwa baada ya muda mrefu. Hata hivyo, hii haimaanishi kwamba maadili na mitazamo si muhimu au haviwezi kutathminiwa. Hivi pia vinaweza kutathminiwa ingawa si rahisi kama ujuzi, ufahamu na stadi ambavyo vinatathminiwa kupitia kwa mijarabu na mitihani. Mitazamo na maadili yanaweza kutathiminiwa baada ya muda kupitia kuchunguza na kushirikiana na mwanafunzi.

## Sherehe

| Istilahi | Fasili |
|---|---|
| **mtaala wa umilisi** | Ni ule mtaala ambao unakuza uwezo wa wanafunzi wa kutumia, kwa kujiamini, maarifa waliyojifunza, katika hali mbalimbali |
| **uhusishaji** | Ni mfumo wa kufundishia kwa kuhusisha mbinu na tajriba za ujifunzaji zinazofaa mahitaji, mapendeleo na uwezo wa kila mwanafunzi. |
| **stadi za msingi** | Stadi ambazo hukuzwa katika masomo yote ambazo huwezesha ujifunzaji wa masomo hayo. Stadi hizi pia huwezesha vijana kufanya kazi za kujikimu maishani. |
| **ujumuishaji** | Ni mkabala wa kupanga tajriba za ujifunzaji ambao humwezesha kila mwanafunzi kujiamini, kuhisi salama, kujihisi anaheshimiwa na amewezeshwa kujifunza kikamilifu. |
| **matarajio ya ujifunzaji** | Ni kauli ambayo hutaja kile ambacho mwanafunzi anastahili kujua, kufahamu, kutumia au kutenda katika kipengele mahsusi cha somo. |
| **sampuli ya tathmini** | Shughuli ambayo humpa mwanafunzi fursa ya kuonesha kiasi cha ujifunzaji ambao amepata kutokana na matarajio mahsusi ya ujifunzaji. Hii ni sehemu ya ufundishaji na ujifunzaji wa kawaida, na isichukuliwe kuwa ni shughuli ya ziada ambayo hufanywa mwishoni mwa mada. |
| **shughuli pendekezwa ya ujifunzaji** | Ni kipengele cha ufundishaji wa kawaida ambacho kitawezesha utathmini wa mwigo kufanyika. |




**CONTACT US:**

National Curriculum Development Centre
Plot M838, Kyambogo.
P.O.Box 7002 Kampala, Uganda
+256-393-112-088
**www.ncdc.go.ug**

ISBN 978-9970-494-95-8

9 789970 494958